

**UWASILISHAJI WA UFEMINISTI KINZANI KATIKA  
KISWAHILI KUPITIA TAFSIRI: TATHMINI YA RIWAYA  
YA *BARUA NDEFU KAMA HII***

**NA**

**MAGDALINE CHEPCHIRCHIR YEGON**

**C50/84059/2012**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI  
YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA  
CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**NOVEMBA, 2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine chochote.

Yegon Magdaline	Chepchirchir	Sahihi	Tarehe
C50/84059/2012		.....	.....
(Mtahiniwa)			

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi mteuliwa na Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Sahihi	Tarehe
.....	.....
Dkt. Zaja Omboga	
(Msimamizi)	

## **TABARUKU**

Natabaruku kazi hii kwa mamangu mpendwa Rael Byegon na babangu Jackson Byegon kwa kunilea na kuniauni kila nilipohitaji msaada wao wakati wa masomo yangu. Naitabaruku pia kwa mume wangu Isaac Kanda kwa kunitia moyo nilipokuwa masomoni na hasa wakati wa kufanya utafiti huu. Tabaruku kuu zaidi ni kwa Ashlynn Cherop, huenda akakosa kufahamu kwa sasa lakini uwepo wake tu ulitosha kunipa hamasa katika masomo yangu.

## **SHUKRANI**

Shukrani zangu za dhati zimwendee Mola kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kufikia kiwango hiki katika masomo yangu.

Kazi hii imefanikishwa kutokana na juhudi na ukarimu wa watu kadhaa. Natoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu; Prof. Zaja Omboga kwa kuniongoza na kunikosoa na kunipa ushauri nilipofanya utafiti wangu. Namshukuru kwa kunirekebisha kwa uangalifu na kuwa subira nami. Mola awabariki. Shukrani zangu ziwaendee wahadhiri wangu wote katika idara ya Isimu na Lugha niliowahi kuwa chinina ufundishaji wao; Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Zaja Omboga, Prof. Iribe Mwangi, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. John Habwe, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri na Dkt. Mungania kwa kuchochea fikra zangu. Mchango wenu wenu wa kiusomi kwangu hauwezi kupuuzwa.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu Marisya, Kanyange, Nyamemba, Zani na Wanjala, Sito, Nyandhiwa na Kilonzo tuliokuwa pamoja katika kipindi cha masomo yangu. Shukrani zangu pia zinamwendea Mume wangu Isaac Kanda kwa kunishika mkono na kunitia moyo nilipokuwa masomoni. Nawashukuru Dan Oyuga na Lily Oyuga kwa msaada wao usio na kifani. Nawashukuru pia Noah, Janet na Alex kwa kuniauni kila nilipowahitaji na kunifaa kwa njia moja au nyingine. Mungu awape baraka tele.

Natoa shukrani zangu kwa wazazi wangu; Jackson Byegon na Rael Byegon kwa kunilea na kunishauri. Nawashukuru dada zangu Beatrice na Nelvine na kaka zangu Evans na Julius; hamkuchoka kunitakia mema na kunitia moyo. Sitamsahau mwajiri wangu, kwa kuniruhusu niendeleze masomo yangu. Mola awajalie baraka tele.

## **IKISIRI**

Tasnifu hii imeshughulikia uwasilishaji wa ufeministi kinzani katika Kiswahili kupitia tafsiri kwa kujikita katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Tulilenga kuchunguza uelewa unaoibuliwa na masuala ya ufeministi katika Kiswahili na kuchunguza namna ufeministi kinzani unajibainisha katika riwaya ya Barua Ndefu Kama Hii kasha kuhitimisha kwamba ufeministi kinzani unafikishwa hadi fasihi ya Kiswahili kupitia Kiswahili. Kwa kuegemea nadharia ya ufeministi wa Kiafrika na ya ulinganifu amilifu tulichunguza masuala ya ufeministi yaliyoibua ufeministi kinzani kama; usasa na ukale wa ndoa, usasa na ukale wa elimu, usasa, mahusiko ya wanandoa katika ulezi, changamoto za kuacha desturi na kukumbatia elimu na usasa na nafasi za uongozi, na kuchunguza mahusiano ya wahusika riwayani ambayo yanasababisha majukumu na misimamo inayokinzana ya wanawake kuhusu masuala ya kifeministi kama; mahusiano baina ya Aisatu na Ramatulayi kwa upande mmoja na Binetuu, Bibi Mama- mkwe na Shangazi Nabu kwa upande ule mwingine. Matokeo yetu yalidhihirisha kuwa upo uelewa kinzani wa masuala ya kifeministi katika fasihi ya Kiswahili. Ufeministi huu kinzani hujitokeza katika mawasilisho kinzani ya masuala ya kifeministi na mawasilisho ya mitazamo kinzani ya wanawake kuhusu masuala ya kifeministi katika riwaya. Hatimaye tumeweza kuhitimisha kwamba maudhui haya ya ufeministi kinzani yamefikishwa katika fasihi ya Kiswahili kupitia tafsiri.

# YALIYOMO

UNGAMO.....	i
<b>TABARUKU.....</b>	<b>ii</b>
<b>SHUKRANI.....</b>	<b>iii</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>iv</b>
<b>VIFUPISHO .....</b>	<b>viii</b>
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.0 Usuli wa Mada .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	5
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	8
1.4 Nadharia Tete.....	8
1.5 Sababu za Kuchagua Mada hii.....	8
1.6 Upeo na Mipaka.....	11
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	12
1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Ufeministi Kinzani.....	13
1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Tafsiri na Uhawilishaji wa Maana .....	17
1.8 Msingi wa Nadharia.....	21
1.8.1 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika .....	21
1.8.2 Nadharia ya Ulinganifu Amilifu .....	28
1.9 Mbinu za Utafiti.....	30

1.10 Hitimisho.....	32
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>33</b>
<b>MAWASILISHO KINZANI YA MUSUALA YANAYOWAHUSU WANAWAKE</b>	<b>33</b>
2.0 Utangulizi.....	33
2.1 Utamaduni na Usasa wa Elimu.....	35
2.2 Suala la Unyumba.....	38
2.3 Usasa na Ukale wa Ndoa .....	40
2.4 Mpito na Mvutano wa Vizazi .....	42
2.5 Wajibu wa Wanandoa katika Ulezi.....	43
2.6 Usasa na Ukale wa Suala la Malezi .....	45
2.7 Suala la Uhuru.....	46
2.8 Suala la Uhuru wa Kiuchumi na Utegemezi wa Kiuchumi .....	49
2.9 Hitimisho.....	51
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>52</b>
<b>WAHUSIKA: MISIMAMO, MAAMUZI NA MASUALA YA KIFEMINISTI YANAYOENDELEZWA KATIKA MAHUSIANO YAO.....</b>	<b>52</b>
3.0 Utangulizi.....	52
3.1 Mahusiano baina ya Ramatulayi na Aisatu; Usasa, Uhuru, Uhuru wa Kiuchumi, Ujitambuzi na Uwajibikaji.....	55
3.2 Mahusiano baina ya Ramatulayi, Binetuu na Nabu Mdogo; Usasa na Ukale wa Ndoa na Usasa na Ukale wa Elimu .....	58

3.3 Mahusiano baina ya Ramatulayi na Aisatu na Bibi Mama-Mkwe Pamoja na Shangazi Nabu; Usasa na Ukale wa Ndoa, Usasa na Ukale wa Malezi, Mvutano wa Vizazi, Changamoto za Kuacha Ukale na Kukumbatia Usasa na Usasa na Ukale wa Elimu.....	60
3.4 Mahusiano baina ya Aisatu na Ramatulayi na Waume wao; Mivutano ya Usasa na Ukale wa Ndoa na Jukumu la Wanandoa katika Ulezi.....	63
3.5 Mahusiano baina ya Ramatulayi na Farmata; Ukale wa Ndoa, Ndoa ya Mitaala na Ulezi.....	66
3.6 Mahusiano baina ya Ramatulayi na Daba; Usasa wa Ndoa, Ujitambuzi wa Mwanamke, Kushiriki kwa Mwanamke katika siasa na Uongozi, Majukumu ya Unyumba na Uhuru wa Mwanamke .....	67
3.7 Mahusiano baina ya Ramatulayi Tamsir na Imamu; Ndoa za Mitaala, Ubabedume Kutowajibika kwa Wanaume katika Ulezi .....	70
3.8 Mahusiano baina ya Ramatulayi na Dauda Diengi; Ushirikishwaji wa Wanawake katika Siasa .....	71
3.9 Hitimisho.....	73
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>74</b>
<b>HITIMISHO .....</b>	<b>74</b>
4.0 Utangulizi.....	74
4.1 Kuhusu Madhumuni ya Utafiti .....	74
4.2 Upimaji wa Nadharia Tete .....	75
4.3 Changamoto za Utafiti .....	78
4.4 Mapendekezo .....	79
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>80</b>



## **VIFUPISHO**

LC- Lugha Chanzi

LL- Lugha Lengwa

HC- Hadhira Chanzi

HL- Hadhira Lengwa

## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 USULI WA MADA**

Tafsiri zimefanywa ili kunufaisha lugha mbali mbali ulimwenguni tangu zamani. Mwanzoni tafsiri za kidini zilifanywa; Biblia ilitafsiriwa kutoka Kihebrania hadi Kilatini miaka ya 347-420. Fasihi ya Kiswahili imefaidika kutokana na tafsiri ngeni kuanzia mwaka wa 1652 ambapo tafsiri ya Utenzi wa Hamziya ulioandikwa kwa Kiarabu ulitafsiriwa kwa Kiswahili na Said Aidarus mnamo mwaka wa 1749. Tangu hapo, tafsiri nyingi za Kiswahili zimefanywa zikiwemo za riwaya ya *Mashimo ya Mfalme Suleiman* (1929), *Kisiwa Chenye Hazina* (1965), *Safari za Gulliver* (1966), *Visa Vya David Copperfield* na *Shamba la Wanyama* (1967). Riwaya hizi ziliingiza maudhui ngeni katika fasihi ya Kiswahili. Mifano hii ni ithibati muhimu ya tafsiri kunufaisha lugha na hata fasihi yake. Kufikia mwaka wa 1994 riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* ambayo ni tafsiri ya kifasihi ya *Une Si Longue Lettre* (1979) ilitafsiriwa.

Tafsiri ya kifasihi ni shughuli ya kitafsiri inayonufaisha fasihi ya lugha; shughuli yenyewe inahusu uhawilishaji wa maana- hasa yenye wasifu wa kifasihi- katika lugha chanzi (tangu hapa LC) hata kama ufasiri wake ni wenye utata au ukinzani. Tafsiri ya kifasihi hufanikishwa na uhawilishaji wa maana. Kwa sababu hii, tafsiri hii basi ni shughuli muhimu inayohakikisha kwamba maana ya kifasihi- hii ni pamoja na maudhui na falsafa ya kifasihi- inayojitokeza katika LC imefikishwa katika lugha lengwa (tangu hapa LL). Maelezo haya yanaibua dhana muhimu katika utafiti wetu ya uhamaji au uhawilishaji wa maana katika shughuli ya tafsiri

Tafsiri imekuwa njia muhimu na mkakati mahususi wa kuhawilisha mambo mengi kati ya tamaduni, lugha na fasihi zao. Hii ni njia moja ambayo kupitia kwayo fasihi za kiulimwengu zimenufaishwa na kuimarishwa na maendeleo ya kifasihi kutoka fasihi nyingine. Tafsiri imewezesha kuhawilishwa kwa mbinu za utunzi wa fasihi, kuhawilishwa kwa mitindo ya kiuandishi, motifu za kifasihi, mikakati ya uumbuji wa wahusika, uhawilishaji wa lugha kwa njia ya msamiati, istilahi, dhana, falsafa na maudhui. Tafsiri zimeweza kujenga vielelezo vya uigaji na ujarabati katika fasihi.

Kwa jumla, mambo haya yote yanayohawilishwa kupitia tafsiri inaelekea kuwa maudhui ndiyo yamehawilishwa kwa wingi. Uchanganuzi wa ukuaji wa fasihi ya Kiswahili kihistoria una ithibati nyingi zinazoonyesha jinsi maudhui ya aina mbalimbali yalivyofikishwa katika fasihi ya Kiswahili kupitia kwa tafsiri. Kwa mfano, kutafsiriwa kwa riwaya ya *Mine Boy* kama *Mchimba Madini* kuliwezesha kufikishwa katika fasihi ya Kiswahili maudhui ya utetesi wa uhuru kutokana na vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe. Vile vile, kutafsiriwa kwa riwaya ya *King Solomon's Mines* kama *Mashimo ya Mfalme Suleiman* kuliwezesha baadhi ya maudhui yakiwemo yale ya mivutano baina ya sayansi na ushirikina kufikia fasihi ya Kiswahili.

Hivyo hivyo, kutafsiriwa kwa riwaya ya Mariama Ba *So Long a Letter* kama *Barua Ndefu Kama Hii*, kuliwezesha kuhawilishwa kwa maudhui ya aina nyingi hadi katika fasihi ya Kiswahili. Riwaya hii imewezesha kuwepo, kwa sasa, kwa maudhui mapya pamoja na kuwezesha kuimarishwa kwa maudhui yaliyopo katika fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, maudhui kuhusiana na masuala ya ndoa za mitaala, masuala ya ndoa na unyumba, ukewenza, ulezi wa watoto, usasa, usasa wa ndoa na migongano yake na ukale

wa ndoa hasa katika jamii iliyo katika mpito ni baadhi ya maudhui ambayo yameweza kuimarishwa. Masuala haya ya unyumba, usasa, usasa na ukale wa ndoa, wajibu na mahusiko ya wanandoa katika ulezi, nafasi za uongozi, changamoto za kuacha desturi na kukumbatia elimu na usasa, yanaibua masuala ya ufeministi.

Suala la ufeministi limewahi kushughulikiwa katika fasihi ya Kiswahili kwa njia nyingi japo kwa kiasi kikubwa tafiti nyingi zina mwegemeo wa kukariri mambo yale yale; haki za wanawake, ukombozi wa wanawake, usawa kwa wanawake, mateso na dhuluma dhidi ya wanawake, udunishaji wa hadhi ya wanawake, utetezi wa wanawake dhidi ya ukandamizaji katika jamii yenye mifumo iliyodhibitiwa na wanaume. Masuala haya yote yanaangaliwa kama mawanda ya mijadala ya ufeministi na vinginevyo kama nguzo za kimsingi katika masuala ya ufeministi na kutokana nayo yote kwa jumla kunaibuka maswali; je, fasihi ya Kiswahili ina uelewa mmoja wa ufeministi? Je, inawezekana kukawa kuna uelewa kinzani wa masuala ya kifeministi? Ukinzani huo wa kifeministi unafafanuliwa kwa njia gani na unajibainisha kwa njia gani?

Kuibuka kwa maswali haya kunatokana na ukweli kwamba katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*, kuna mawasilisho kinzani ya masuala yanayowahusu wanawake kwa upande mmoja na mawasilisho ya mitazamo kinzani ya wanawake ndiposa tukashawishika kuchunguza mada yetu ya mahusiko ya tafsiri katika uwasilishaji wa ufeministi kinzani katika Kiswahili kupitia tafsiri kwa kujikita katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* ambayo ni tafsiri ya Profesa Maganga ya *So Long a Letter* iliyoandikwa na Mariama Ba.

Mtu anapofuatiliafafanuzi za kinadharia na kiusomi zilizoko juu ya uelewa wa dhana nzima ya ufeministi katika fasihi ya Kiswahili, kunaibuka mikinzano na mivutano mingi. Kwa mfano, kama dhuluma kwa wanawake kutokana na mifumo ya kibabedume Mutua (2007); kama msingi, msukumo na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kisiasa na kiuchumi Wamitila (2008); kama ujidhihirishaji wa ubaguzi wa kijinsia na utosawa wa mahusiano ya kiuchumi, kidini na kijamii kati ya wanawake na wanaume Masibo (2009); ufeministi umefafanuliwa kama nadharia ya fasihi inayojishughulisha na utetezi wa wanawake dhidi ya ukandamizaji Swaleh (2011); ufeministi kama madai ya uanamama, utambuzi wa uwezekano na mwito na kuwapa wanawake nafasi sawa na wanaume katika nyanja za kijamii, kisiasa, kielimu, na kidini Ifejirika (2014); ufeministi kama mwito wa kimapinduzi wa mapigano dhidi ya wanaume na mapigano dhidi ya utosawa wa wanaume, madai ya uhuru usiodhibitiwa wa wanawake, n.k.

Kwa hivyo, inabainika kwamba dhana ya ufeministi na ufafanuzi wake katika usomi wa fasihi ya Kiswahili ni suala changamano. Uchangamano huu wa mambo kama vile usasa na ukale wa masuala ya ndoa, utamaduni na usasa wa elimu, mpito na mvutano wa vizazi, uhuru na utegemeaji, uhuru wa kiuchumi na utegemezi wa kiuchumi, usasa na ukale wa suala la malezi, nafasi za uongozi kwa wanawake na wanaume, changamoto za kuacha desturi na kukumbatia elimu na usasa au uamuzi wa kushikilia desturi na ukale ni uhalisi unaoakisiwa katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Swali linaloibuka kutokana na muhtasari huu wa mambo ni; uhawilishaji wa mambo changamano kama haya hadi fasihi ya Kiswahili una maana gani kuhusiana na ufasiri wa ufeministi.

Suala zima la ufeministi kinzani haliwezi kuelezwa kwa kifupi kwani hufumbata mambo tofauti tofauti. Ufeministi kinzani sio tu hali ya wahusika kuwa na falsafa, mielekeo, misimamo inayokinzana au kuchukua hatua zinazoelekea kukinzana kuhusu masuala ya kifeministi bali pia huhusu pale ambapo ufeministi unashindwa kueleza iwapo mwanamke ni huru au mtegemezi; ni mhitaji au anayejiweza; kama anajitegemea basi husemwa kuwa anayejiweza na iwapo ni mhitaji basi anahitaji mwanamume amkinge Mansfield (2014). Haya yote pamoja na mawasilisho kinzani ya masuala yanayowahusu wanawake kwa upande mmoja na mawasilisho ya mitazamo kinzani ya wanawake.

Mada yetu; ‘Uwasilishaji wa Ufeministi kinzani Katika Kiswahili Kupitia Tafsiri: Tathmini ya Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*’ inatoa mchango wake katika eneo la fasihi tafsiri ya Kiswahili kwa kuchunguza suala la mahusiko ya tafsiri katika uhawilishaji wa maudhui na falsafa hadi kufikia LL hata kama yanazua uelewa kinzani katika lugha chanzi LC. Matumaini yetu ni kwamba uchunguzi wetu umechangia kukuza na kupanua maudhui katika eneo la fasihi tafsiri na kusababisha fasihi ya Kiswahili kuingia katika mawanda mapya ya kimaudhui.

## **1.2 TATIZO LA UTAFITI**

Utafiti huu ulijishughulisha na suala la kufasiri ufeministi kwa kadri unavyoibuliwa na masuala changamano ya kimaudhui yanayojitokeza katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Uchanganuzi wa kimaudhui wa *Barua Ndefu Kama Hii* unadhihirisha masuala mengi ya kimsingi ambayo kwa njia moja au nyingine yanahusiana na ufeministi. Masuala haya yanalizungukia suala la mahusiano kati na miongoni mwa wahusika, wake wa kwanza; Ramatulayi na Aisatu kwa upande mmoja, na mahusiano yao na waume zao, mama

mkwe zao na wakewenza wao; Nabu mdogo na Binetuu kwa upande mwingine. Hatimaye kuonyesha kuwa mambo haya yanachangiana kuibua maudhui ya ufeministi yaliyo kinzani na kuhitimisha kwamba maudhui haya-kwa ukinzani wao-yanahawilishwa hadi fasihi ya Kiswahili kwa kupitia tafsiri.

Mahusiano yao kuhusiana na hadhi zao za kielimu, kikazi na kijamii katika hali za mivutano ya kitamaduni na mpito wa wakati. Maamuzi yao kuhusiana na masuala mbalimbali katika jamii yao; usasa, elimu na uhuru kwa upande mmoja na mivutano ya kitamaduni, kidini na kifamilia kwa upande mwingine. Uchangamano huu wa kimahusiano unapodadisiwa kwa kina na kutumiwa kama msingi wa kufafanua ufeministi unaibua uchangamano wa uelewa kuhusu ufeministi kwa jumla. Uanuwai huu wa kimahusiano ulichochea haja ya kutaka kuelewa ni kwa jinsi gani masuala haya changamano yanachangia kuibua ufeministi kinzani katika fasihi ya Kiswahili.

Kimsingi katika utafiti huu tulitaka kudai kwamba tafsiri ni njia na mkakati wa kimsingi katika uhamishaji na uhawilishaji wa maudhui, hivi kwamba ukweli huu unapochanganuliwa katika miktadha ya riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*, kuna ithibati kwamba tafsiri imehusika pakubwa katika uhawilishaji huo wa maudhui na ufasiri unaambatana na maudhui hayo. Kuna ithibati za aina mbalimbali katika riwaya hii zinazoonyesha kwamba tafsiri imehusika pakubwa katika uhawilishaji wa mambo yaliyo na wasifu wa kifeministi, fikira za kifeministi, mienendo ya kifeministi hata njia na mifumo ya harakati za kifeministi, mifumo ya kifeministi ya kufikiri, kuwaza, kupanga mambo, kutatua matatizo ya kifeministi, matumizi ya mitindo ya kujieleza ya kifeministi. Hii ni ithibati tosha ya kwamba tafsiri inafaidi lugha na fasihi yake.

Msukumo wa kutaka kuchanganua mahusiko ya tafsiri katika uhawilishaji wa maudhui ulitokana na ukweli kwamba fasihi ya Kiswahili imesheheni kazi nyingi za kifasihi zilizo na maudhui yaliyohawilishwa kwa njia ya tafsiri. Tunataka kuhoji kwamba tafsiri ni mkakati ambao haunufaishi tu lugha bali pia unanufaisha hata na fasihi yake. Malengo haya tunataka kuyatekeleza kwa kujikita katika kuchanganua usawiri wa wahusika na mahusiano yao, majukumu ya wahusika hawa pamoja na miktadha ya mitagusano ya wahusika hawa katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Katika kuangazia mambo haya, hatimaye tulitarajia kuonyesha jinsi yanavyochangiana kuibua maudhui ya kifeministi yaliyo kinzani.

Kwa hivyo, utafiti unaangazia mahusiko ya tafsiri katika uhamaji na uhawilishaji wa maudhui ya fasihi za kiulimwengu na fasihi ya Kiswahili. Tunaafiki kwamba ndio, masuala ya ufeministi yapo katika fasihi ya Kiswahili lakini je, masuala haya yana uelewa mmoja? Je, inawezekana kukawa kuna uelewa kinzani wa masuala ya kifeministi? Ikiwa upo, ukinzani huo wa kifeministi unafafanuliwa kwa njia gani na unajibainisha kwa njia gani? Kuibuka kwa maswali haya kunatokana na ukweli kwamba katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*, kuna mawasilisho kinzani ya masuala yanayowahusu wanawake kwa upande mmoja na mawasilisho ya mitazamo kinzani ya wanawake. Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* iliyotafsiriwa na Profesa Maganga kutoka kwa riwaya ya *So Long a Letter* iliyoandikwa na Mariama Ba ni mfano mwafaka wa uhawilishaji wa maudhui katika fasihi tafsiri ya Kiswahili.



### **1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI**

Utafiti wetu utakuwa na madhumuni yafuatayo:-

- i. Kuchunguza uelewa unaoibuliwa na masuala ya ufeministi katika fasihi ya Kiswahili.
- ii. Kuchunguza namna ufeministi kinzani unavyojibainisha katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*.
- iii. Kuthibitisha kwamba ufeministi kinzani unafikishwa katika fasihi ya Kiswahili kupitia tafsiri.

### **1.4 NADHARIA TETE**

Utafiti wetu utakuwa na nadharia tete zifuatazo:-

- i. Masuala ya ufeministi yanaibua uelewa kinzani katika fasihi ya Kiswahili.
- ii. Ufeministi kinzani unajibainisha kupitia nafasi, majukumu na misimamo ya wahusika wa riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*.
- iii. Ukinzani wa ufeministi unafikishwa katika fasihi ya Kiswahili kupitia tafsiri.

### **1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII**

Tulichagua kutafitia somo hili ili kuchunguza mahusiko ya tafsiri katika uhawilishaji wa maana hadi LL hata ingawa maana yenyewe ina uelewa kinzani katika LC. Somo hili tulilitafitia ili tupate kuchangia katika eneo la kiusomi la fasihi tafsiri kwa kujikita katika fasihi tafsiri ya Kiswahili kisha kuonyesha mchango wa tafsiri katika kuyahawilisha

baadhi ya maudhui haya katika Kiswahili. Uchunguzi wetu umeonyesha kwamba ipo ithibati chungu nzima kwamba fasihi ya Kiswahili imetajirishwa na tafsiri.

Utafiti na usomaji wetu umedhihirisha ya kwamba tafsiri ina mchango katika ukuzaji wa lugha na hata fasihi yake. Utafiti wetu pia umeonyesha kwamba masuala ya ufeministi yamejitokeza katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* kwa namna fulani inayochochea uchunguzi wetu. Mambo haya yalitulazimu kufanya uchunguzi wa nafasi, misimamo, mahusiano na mitagusano ya wake wa kwanza na wanawake wengine wanaowaunga mkono kuhusu masuala ya ufeministi katika riwaya teule kwa upande mmoja na wake wenza wao, wakwe zao pamoja na waume wao na ndugu zao, viongozi wa kidini na wanasiasa kwa upande mwingine ili kuonyesha kwamba yote yanachangiana kuibua maudhui ya ufeministi kinzani hatimaye kuonyesha kwamba maudhui haya yanahawilishwa hadi fasihi ya Kiswahili kupitia tafsiri.

Muktadha wa utamaduni wa Kiafrika unashikilia muungano wa kijamii, humtaka mwanamke aafikiane na itikadi na kanuni za jamii, humtaka akubali majukumu yake, aafiki mila na itikadi chukulizi, humtambua mwanamke kwa sifa zisizokadirika na kuendeleza ujitambuzi na ung'amuzi wa Kiafrika. Ufeministi kwa upande wake hushikilia kwamba mwanamke ajitambue kama mtu binafsi, humtaka mwanamke atambulike kutokana na tajriba zake wala si mahusiano ya kijamii, humtaka mwanamke atambue uwezo wake na matamano yake, aweze kujiamulia maadili yake, awe na kiwango cha uwezo wa kifedha na kuendeleza ujitambuzi na ung'amuzi wa kibinafsi.

Mwanamke basi anaweza kubali kuwekwa chini ya udhibiti wa utamaduni na maamuzi na matendo yake kupingwa kwa misingi ya kidini na kitamaduni badala ya hatua,

matamano na mafanikio yake kama mtu binafsi kutambuliwa. Kwa upande mwingine mwanamke anaweza kukataa kudhibitiwa na utamaduni au dini na kujitambua mwenyewe kama mtu binafsi mwenye uamuzi huru na mwenye matamano yake kunaibua hali tofauti ya ufeministi. Uchangamano huu wa masuala haya ya ufeministi ndio uhalisia unaoakisiwa katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*.

Sababu nyingine hasa ya kuchagua mada hii ni kwamba zipo tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu mchango wa tafsiri katika ukuzaji wa lugha na fasihi yake zikiwemo za Ruhumbika (1983) na Zaja (2006). Tafiti nyingine zimeshughulikia mada hii kama sehemu ndogo ya mada kuu kama vile, Mutua (2007). Nyingine zimechunguza tofauti za kiisimu na kimuundo baina ya lugha zinazohusishwa katika tafsiri Kihore (1989) na nyingine zikachunguza jinsi lugha chanzi huweza kubadilishwa ili kupata tafsiri timilifu Khamisi (1989). Utafiti huu uliwasilishwa katika kongamano la UNESCO katika kikao chake cha Dar-es Salaam. Zaja (2006) amechunguza riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* kwa upana na undani akiangazia uteuzi wa nadharia katika kuhakiki kazi zilizotafsiriwa, umuhimu wa kuzingatia utamaduni katika kuchunguza kazi za tafsiri, baadhi ya masuala ya ufeministi tuliyoyashughulikia, pia ameshughulikia nafasi waliyopewa waandishi wanawake katika fasihi ya Kiswahili na utanzu ulioteuliwa kuandika riwaya hii kama ulioipa riwaya hii upekee na nafasi kubwa ya kuwasilisha maudhui ya kifeministi.

Zaja amechunguza riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* kwa kutazama mikakati banifu na kiushi katika kushughulikia tafsiri pamoja na matumizi yao katika ufasiri wa matini za kifasihi. Katika uchunguzi wake amesisitiza umuhimu wa kuzingatia utamaduni katika shughuli ya kutafsiri. Pia, zipo tafiti zilizofanywa kwa Kiswahili ambazo

zimeshughulikia mahusiko ya tafsiri katika uhawilishaji wa maana lakini kwa jumla ya usomi wetu hakuna utafiti tunaoujua wa Kiswahili ambao umeshughulikia uhawilishaji wa maana yenye uelewa kinzani kwa mkabala wa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika na ya ulinganifu amilifu katika tafsiri.

Tuliteua riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* kwa kuwa nakala yake asilia iliandikwa katika Kifaransa na imewahi kutafsiriwa kwa lugha kumi na saba ikiwemo Kiingereza. Tafsiri ya Kiingereza ndio imepata kusomwa zaidi kuliko ile ya Kifaransa. Jambo hili limeiwezesha riwaya hii kupokelewa na hadhira pana na hasa ndio sababu tuliyopata ya kuteua tafsiri ya Kiingereza. Isitoshe, tamaduni za lugha ya Kifaransa na Kiswahili zinawasilisha tofauti kuu za kimaudhui kwa hivyo kuwezesha uhawilishaji wa maudhui ngeni katika Kiswahili. Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* ilitafsiriwa kwa mikakati iliyoipa ufanisi mkubwa na imekuwa kama jibu kwa swali la ‘iwapo lugha ngeni inaweza au haiwezi kutafsiri kwa njia toshelevu kile kilichoko katika maudhui tofauti’; swali lililowashughulisha watafiti wengi hapo awali (Gyasi, 2006). Riwaya yenyewe pia ni riwaya tafsiri na imesheni hali mbalimbali za ufeministi kinzani ambazo ni data tuliyochunguza.

## **1.6 UPEO NA MIPAKA**

Utafiti wetu ulichunguza mahusiko ya tafsiri katika uhawilishaji wa maana; tukijikita katika ukinzani uliopo kwenye maana na kuonyesha kwamba tafsiri imehusika katika uhawilishaji wa maana inayojitokeza. Msisitizo wetu ulikuwa kwenye mchango wa tafsiri katika uhawilishaji wa maana kwa jinsi inavyojitokeza katika lugha chanzi. Tulichunguza masuala ya ufeministi yenye ukinzani. Hatukujikita katika uchunguzi wa sifa za wahusika

katika riwaya teule bali tulichunguza msimamo wa; wake wa kwanza, wake wa pili, wakwe zao wa kike pamoja na wanawake wengine wanaowaunga mkono kuhusu masuala ya kifeministi. Isitoshe, tulichunguza nafasi na majukumu ya waume wao na ndugu zao, viongozi wa kidini na wa kisiasa. Tulitumia riwaya tafsiri ya Kiswahili ya *Barua Ndefu Kama Hii* kama riwaya kuu ingawa tulihitajika kusoma na kufanya urejelezi wa hapa na pale wa riwaya ya *So Long A Letter*.

Tulichukua mkabala wa nadharia ya ufeministi wa kiafrika katika uchunguzi wa masuala ya kifeministi na nadharia ya mawasiliano kuchunguza masuala ya uhawilishaji wa maana. Hatukujishughulisha na masuala yote ya ufeministi yanayojitokeza katika riwaya bali tulijishughulisha tu na masuala ya ufeministi kinzani labda tu kufanya urejelezi wa hapa na pale kwa ufeministi. Hatimaye tumeweza kutoa maoni yetu kutokana na uchunguzi ambao tulikuwa tumefanya ili kuonyesha uelewa wa ufeministi katika fasihi ya Kiswahili, namna ufeministi kinzani unavyojitokeza na kutoa maoni kuhusu namna yanavyohawilishwa katika Kiswahili.

## **1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA**

Mada yetu inafumbata mambo mawili makuu; ufeministi kinzani na tafsiri na uhawilishaji wa maana kwa sababu hii tumegawa yaliyoandikwa kwa vikundi viwili. Tumefanya hivi kwa sababu ufeministi kinzani ulizuka kutokana na ufeministi na uhawilishaji wa maana una uhusiano mkubwa na tafsiri kwa kuwa tafsiri huhusisha uhawilishaji wa maana.

### **1.7.1 YALIYOANDIKWA KUHUSU UFEMINISTI KINZANI**

Ufeministi ni tapo la kisiasa, kitamaduni na kiuchumi linalonua kutetea usawa kwa wote na kumkomboa mwanamke. Miller (1990) anaeleza kuwa katika muktadha wa kiafrika, ufeministi unajikita katika misingi ya maadili ya kimapokeo ya kiafrika na kushughulikia jinsia na masuala yanayohusiana nayo katika mazingira ya kijamii na kitamaduni ya Kiafrika. Ufeministi wa mwanzo ulijikita katika njia za kumsaidia na kuinua hali ya mwanamke anayedhalilishwa. Ufeministi kwa sasa unajikita katika ukuzaji zaidi wa hadhi ya kijamii ya mwanamke ambaye tayari ana hadhi nzuri, kuendeleza useja wa hapa na pale na malezi ya mzazi mmoja. Juhudi za ufeministi wa Kiafrika zinajikita katika kumkomboa mwanamke wa Kiafrika kutokana na ukandamizaji wa kitamaduni, kiuchumi na kidini katika jamii inayotawaliwa na ubabedume.

Changamoto zinazowakabili wanawake zinaweza kutofautiana kimaeneo lakini zipo kote ulimwenguni. Changamoto nyingine zimejikita katika dini, jinsia au utamaduni. Jamii mbalimbali zina itikadi zao mbalimbali za kidini, kijinsia na kitamaduni kwa hivyo wanajamii huchukua nafasi na majukumu mbalimbali. Misingi hii tofauti basi husababisha misimamo, mikabala na mitazamo tofauti tofauti ya wanajamii ya kuyashughulikia masuala haya. Zaidi ya hayo, mitazamo hii tofauti imo katika kiini cha kufasiri, kueleza na kuendeleza juhudi za kifalsafa au za kiharakati za masuala ya ufeministi.

Kuwepo kwa tofauti za kimitazamo katika uwasilishaji wa kifeministi katika fasihi kunasababisha uwasilishaji kinzani kuhusiana na masuala ya ufeministi ambapo sambamba na uwasilishaji wa kifeministi kuna uwasilishaji kinzani wa kifeministi

ambao ama; wanawake wanaunga mkono na kuendeleza itikadi zinazomdhalilisha mwanamke au kuzipinga itikadi hizi kama anavyosisitiza Jones (1985) kwamba mwanamke anaelezwa kuwa mhitaji wala si anayejiweza kwa hivyo kumhitaji mwanaume amkinge au kutambua kwamba anajiweza wala hamhitaji mwanaume kumkinga.

Ukinzani pia unaweza kudhihirika pia ambapo ama; mwanamke anamtazama mwanaume kama njia ya kuboresha hadhi yake maishani au kutambua uwezo wake wa kubadili na kuboresha hadhi ya maisha yake kwa juhudi zake mwenyewe. Mwanamke anakubali hali yake ilivyo bila ya kutaka mabadiliko yoyote yafanyike au kuchukua hatua ya kuboresha hali yake na kuleta mabadiliko maishani mwake Stegeman (1974).

Zaja (1986) anadokezea kinaya cha wanawake kuunga mkono itikadi za kurudi nyuma zinazozidisha hadhi yao ambayo tayari imedunishwa katika jamii. Huku hali hii inaweza kuchanganuliwa kama kinaya tu, inaweza pia kudokezea ukinzani inapotazamwa sambamba na maadili ya ufeministi na mwito na nia kuu ya ufeministi unaotaka wanawake kupinga na kukataa kudhalilishwa na kudunishwa. Hali ya ukinzani inajitokeza kwa kuwa kwa upande mmoja mwanamke anahitajika kuitikia mwito wa ufeministi, kujikomboa na kujitambua huku jamii kwa upande wake inamtaka atimize majukumu yake ya kijamii kama mwanajamii wala si kama mtu binafsi na awakilishe maadili ya jamii; hali hizi mbili zinakinzana.

Maelezo haya ya Zaja yanachangia utafiti wetu katika kudokezea uelewa kuhusu ukinzani unaoweza kuibuka kuhusu masuala ya ufeministi yaani; ufeministi kujipinga wenyewe. Kuna uhusiano mkubwa wa maelezo yake na yale ya Mutua (2007) ambayo

yanaelekea kufafanua ukinzani huu zaidi. Akieleza kuwa ufeministi pingamizi umejitokeza katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* sawa na katika *Migogoro* ambapo mhusika msichana; Rukia anaelimishwa lakini baada ya babake kuchekwa na wenzake anajutia hatua hiyo; Musyoka anadokezea kuwa ufeministi umejipinga wenyewe katika hali hii.

Hali hii pia imejitokeza katika *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ambapo Bi. Tukaije anamkataza bintiye kujichagulia mchumba na pale ambapo Bi. Mwatima na Sikitu wanamdharau Hidaya kwamba alikuwa kiruka njia na kwamba alikuwa ameavya mimba. Musyoka ameshughulikia suala la ufeministi kinzani kama sehemu ya mada kuu na ufafanuzi wake wa ufeministi pingamizi unashabihiana na wetu ila tofauti na sisi alichagua msamiati “ufeministi pingamizi” na sisi tuliuita “ufeministi kinzani”. Maelezo yake; sawa na ya Zaja (1986) yanaeleza kinaya cha wanawake kuunga mkono itikadi zinazowadhilisha kwa hivyo kukinzana na maadili ya ufeministi na kujitokeza kama ufeministi kujipinga.

Maelezo haya yaanaafiki ukweli wa maadili ya ufeministi kuwekwa kando katika kushughulikia masuala ya uamuzi wa mwanamke hasa ikiwa uamuzi wenyewe una madhara kwake kwa kushikilia kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Hali hii inasisitizwa na kauli hii; ‘Ufeministi kinzani unajitokeza pale ambapo maadili asilia ya ufeministi yamewekwa pembeni katika kueleza baadhi ya misimamo ya wahusika inayokwenda kinyume na maadili asilia ya ufeministi’ Masibo (2009). Mchango wao ni muhimu kwa utafiti wetu hata ingawa katika utafiti wetu tulichunguza ufeministi kinzani unavyojidhihirisha kupitia nafasi, majukumu na mahusiano ya baadhi ya wanawake na



wanaume katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*; kuhusu hadhi yao ya kikazi, kielimu na kijamii na katika maeneo ya mivutano ya kitamaduni, kidini na kifamilia. Kwa hivyo mchango huu umetupa mwongozo wa kudondoa na kutambua mifano ya hali zinazoshabihiana nazo katika *Barua Ndefu Kama Hii*.

Jones na wengine (1985) anaeleza kuwa ufeministi kinzani unajitokeza pale ambapo mwanamke anadaiwa kuwa ambaye ni mhitaji na hivyo kumhitaji mwanamume amkinge na kwa upande mwingine kudaiwa kwamba mwanamke-sawa na mwanamume-anajiweza. Hali hizi mbili zinakinzana na kuibua maudhui ya ufeministi kinzani. Maelezo haya ya Jones na wengine yalichangia katika uchunguzi wetu wa usawiri wa masuala tofauti yanayohusu wanawake katika riwaya tuliyoteua. Masibo (2009) akichambua riwaya za Ngugi wa Thiong'o na Alice Walker anaeleza kuwa katika jamii kadhaa ulimwenguni, ubaguzi wa kijinsia unajidhihirisha katika utosawa wa kiuchumi, kisiasa, kidini na kijamii wenye madhara kwa wanawake. Kazi hii imetufaa kama darubini katika kueleza majukumu, nafasi, matendo na hata mawazo ya wahusika katika kazi ya fasihi tutakayoshughulikia.

Kwa mujibu wa Ifejirika (2014) akichunguza ufeministi kama kisasili anaeleza kuwa katika kiwango fulani, ufeministi uligeuka na kuwa mwito wa kimapinduzi wa mapigano dhidi ya wanaume, mapambano ya usawa, madai ya uhuru usiodhibitiwa wa wanawake na udhamini wa malezi ya mzazi mmoja. Mtazamo huu unakinzana na mawazo asilia ya utetezi wa ufeministi ambayo yalidai haki kwa wanawake, hadhi bora kwao kijamii na haki za wanawake kisiasa. Mawazo haya ya Ifejirika yanaelezea ukuaji wa ufeministi.

Ufeministi kinzani ulitokana na kuwepo Kwa ufeministi, Kwa hivyo, mawazo ya Ifejirika yalinufaisha uchunguzi wetu hasa kuhusiana na msingi wa kinadharia.

Yote tuliyotaja yanafafanua ufeministi kinzani pamoja na suala zima la ufeministi wa Kiafrika kuzua ukinzani unapotazamwa mkabala wa madai ya ufeministi katika muktadha wa mila, itikadi na utamaduni wa Kiafrika. Ukweli huu unatokana na madai ya ufeministi unaonua kumpa mwanamke uhuru, kumpa ujitambuzi wa kibinafsi na kumkomboa kutokana na dhuluma na udhibiti katika jamii yenye ubabedume. Kwa upande mwingine mila, itikadi na utamaduni wa Kiafrika humtaka mwanamke ajitambue katika mipaka ya utamaduni wa kiafrika, aafikiane na maadili ya Kiafrika na kutekeleza majukumu yake anayopewa na jamii kulingana na utamaduni wa Kiafrika. Hali hizi mbili zinadhihirika kama ufeministi kujipinga Stegeman (1974) na Jones (1985) Ni muhimu kutambua kwamba wanawake huchukua nafasi na majukumu mbali mbali katika jamii, hukabiliana na matatizo tofauti na kutangamana na kuhusiana na watu tofauti maishani. Kwa sababu hii huchukua mielekeo na misimamo au hatua tofauti kuhusiana na masuala ya kifeministi yanayowakabili.

### **1.7.2 YALIYOANDIKWA KUHUSU TAFSIRI NA UHAWILISHAJI WA MAANA**

Tafsiri ni shughuli ya kimawasiliano inayuhusu mchakato wa uhawilishaji wa maana kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Nida (1969) anaeleza kuwa tafsiri ni shughuli inayohusisha uzalishaji katika LL wa ulinganifu asilia wa ujumbe ulio karibu sana na ujumbe wa LC; kwanza kimaana na pili kimtindo. Larson (1984) anaeleza kuwa tafsiri ni uhawilishaji wa maana ya LC hadi lugha pokezi; lugha lengwa (LL) naye Newmark (1988) anaeleza kuwa tafsiri ni kusababisha maana ya matini kujitokeza katika lugha

nyingine kwa jinsi ambavyo mwandishi alinuia matini iwe; ni uhawilishaji wa maana ya lugha chanzi (LC) na kuingizwa katika lugha pokezi (lugha lengwa; LL) Newmark (1988).

Nida alichangia pakubwa katika eneo la tafsiri kwa kupendekeza ulinganifu amilifu ambao una nia ya kuleta katika HL athari sawa na ile ya HC na unatilia maanani utamaduni wa lugha lengwa. Mchango huu wa Nida, Newmark na Larson ulikuwa kama darubini katika uchunguzi wetu tuliposhughulikia mahusiko ya tafsiri katika uhawilishaji wa maana kama shughuli kuu inayofanyika katika tafsiri ambapo tutatilia maanani umuhimu wa ulinganifu aliotaja Nida, uhawilishaji alioeleza Larson na kuzingatia kwamba ML hujitokeza kwa jinsi ambavyo mwandishi alinuia kwa maelezo ya Newmark.

Lefevere (1975) anaeleza kuwa tafsiri huweza na aghalabu huhitajika kutekeleza jukumu maalum katika kukuza, kustawisha, kupanua na kufasiri fasihi. Kauli hii ya Lefevere inakubaliwa na Ruhumbika (1983) akieleza kuwa faida kuu ya tafsiri ya vitabu vya waandishi mashuhuri wa lugha inapatikana katika kupanua kiwango cha fasihi yetu katika karatasi yake ya pili. Maelezo haya yaloichangia kuonyesha umuhimu wa mchango wa tafsiri katika fasihi, na kwa kupitia haya tuliweza kuthibitisha uhawilishaji wa maana kama mchakato unaofanikisha tafsiri.

Kufikia miaka ya themanini mabadiliko yaliingizwa katika usomi wa tafsiri ambapo kuliibuka “mwelekeo wa kitamaduni” unaodhihirisha kwamba uchunguzi wa tafsiri umetoka kwenye msingi wa kimapokeo wa kiisimu na kiujumi na kuingia kwa mtazamo wa kitamaduni. Msingi huu wa kitamaduni unaonyesha kwamba shughuli ya tafsiri si

uhawilishaji sahili tu baina ya lugha tofauti bali ni shughuli inayohusiana sana na mambo ya kiziada ya kimatini kama vile, siasa, uchumi, utamaduni na itikadi Bassnet na Lefevere (2001). Ni kutoka mchango huu wao ndipo tulipata umuhimu wa kuzingatia kipengele cha utamaduni katika utafiti wetu. Mabadiliko haya yanaendelewzwa katika kazi ya Toury (1995) anapoeleza kuwa tafsiri ni matini inayojaza pengo katika utamaduni lengwa. Vile vile, ni uwakilisho wa matini iliyokuwepo awali ya lugha chanzi inayowajibikia utamaduni tofauti. Kauli hii ilichangia katika utafiti wetu kwa kuwa katika uchunguzi wetu utamaduni wa matini lengwa ulipewa nafasi kubwa katika ufasiri wa maana.

Venuti (1995) anajikita zaidi katika ufundishaji wa tafsiri, ufasiri wake na lengo la ufundishaji wa fasihi tafsiri ambalo anasema kwamba ni kuelewa tofauti za kiisimu na za kitamaduni. Anaendeleza kwamba ufundishaji wa tafsiri haujishughulishi tu na tofauti baina ya matini chanzi na matini lengwa bali pia tofauti zilizopo kwenye matini lengwa yenyewe na kutafuta suluhu katika mijadala inayoendelezwa kuhusu wingi wa tamaduni. Hermans (1985) anashughulikia juhudi za kiusomi za tafsiri katika uchunguzi wa fasihi kutengwa, kupuuzwa na kupewa nafasi ndogo sana katika fasihi, anadokezea mtazamo finyu wa kuchukulia kwamba fasihi tafsiri hazina maana kama kazi asilia na mtazamo kwamba kazi asilia ni bora zaidi kuliko tafsiri yake kwa kuishia kwa uchujaji wa tafsiri zozote zinazoibuka za kazi asilia na udhihirishaji wa upungufu wa tafsiri zinazoibuka.

Zipo tafiti zilizofanywa kuhusu mchango wa tafsiri katika fasihi kwa kutumia nadharia mbali mbali lakini nyingi zimefanywa katika Kiingereza, nyingine zimechunguza uteuzi

wa nadharia mwafaka ili kusuluhisha matatizo ya tafsiri na namna ya kuyatatua, nyingine zinakubali kwamba tafsiri ina mchango lakini kazi zilizoibuka kutokana na tafsiri zina upungufu. Kihore (1989) na Khamisi (1989) katika makala yao yaliyowasilishwa katika kongamano la Unesco-Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam wameshughulikia tofauti za kiisimu na kimuundo baina ya lugha zinazohusishwa katika tafsiri na jinsi lugha chanzi huweza kubadilishwa ili kupata tafsiri timilifu mtawalia. Hata hivyo sisi tulifanya uchunguzi wetu pasi na kuyapa uzito mambo ya kiisimu na ya kimuundo.

Utafiti wa Zaja (2006) unatafuta kutathmini upya kinadharia tafsiri za kifasihi katika Kiswahili kwa nia ya kupendekeza njia tofauti tofauti za kutumia nadharia zinazofaa, kusoma na kufasiri fasihi tafsiri za Kiswahili. Zaidi, anaeleza kwamba matini tafsiri huweza kusomwa, kufafanuliwa au hata kutolewa nadharia kwa misingi iliyo nje ya mifumo na miundo ya urasmi. Kauli yake hasa kwamba tafsiri inafaa kuwa zalishi kimatini, kitamaduni, na kipedagogia Kwa hivyo huhitaji kuzingatia hali zake za kimuktadha, kimatini na hata zisizodumu zinazozunguka matini yoyote ile. Anachangia kwamba tafsiri inapaswa kuwa uhawilishaji wa kitamaduni

Lugha na fasihi ya Kiswahili ina historia ndefu ya kujadiliana maana kutokana na matini ngeni kuanzia tafsiri ya mashairi ya Kiarabu yanayosifika Mazrui (2007). Uzoefu huu hufungua matini ngeni kwa hadhira pana zaidi Vierke (2009) na kwa hali hii kuiweka wazi riwaya ya Mariama Ba iliyoandikwa kiasilia katika Kifaransa kwa hadhira isiyozungumza Kifaransa kupitia tafsiri zake za Kiingereza na Kiswahili.

Tafsiri inapojishughulisha na tafsiri ya maana ya kifasihi huibua fasihi tafsiri. Zaja (1986) anasema kuwa athari zitokazo nje ziliingia katika fasihi ya Kiswahili na kuifanyia

mabadiliko makubwa kimaudhui na kiumbo katika vipindi mbalimbali kihistoria katika kupanua maudhui. Inakubalika kuwa tafsiri zimetoa mchango mkubwa katika kupanua fasihi ya Kiswahili pamoja na kuinua kiwango chake cha kisanaa. Zaja ameshughulikia fasihi tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili ambamo anazingatia matatizo na athari zake hasa ubora na udhaifu. Hii inahusiana na kazi yetu kwa kuwa sisi tulitumia riwaya ya fasihi tafsiri na kazi yetu ilijikita katika uhawilishaji wa maudhui ya kifasihi na kuchunguza mahusiko ya tafsiri katika uhawilishaji huo.

## **1.8 MSINGI WA NADHARIA**

Omboga (2006) anaeleza kwamba tafiti za kiusomi za tafsiri zinabainisha ukosefu wa msingi wa kuegemea wa kinadharia. Akiendelea, anapendekeza kwamba ujenzi wa msingi wa kinadharia haufai kujikita katika nadharia moja. Kauli hii ilitia nguvu uteuzi wetu wa kinadharia tukitilia maanani kwamba utafiti wetu unahusisha mambo mawili makuu; tafsiri na maudhui ya kifasihi. Kwa sababu hii, utafiti wetu uliongozwa na kuwekewa msingi na nadharia mbili; nadharia ya ufeministi wa Kiafrika na nadharia ya ulinganifu wa maana. Tuliegemea nadharia ya ufeministi wa Kiafrika kwa kushughulikia masuala ya ufeministi na nadharia ya tafsiri ya ulinganifu amilifu katika kushughulikia suala la uhawilishaji wa maana.

### **1.8.1 NADHARIA YA UFEMINISTI WA KIAFRIKA**

Showalter (1977) anadai kuwa ufeministi asilia ulianza kushughulikiwa tangu karne ya kumi na nane katika kazi za wataalam kama Mary Wollestonecraft (1792) wakati *A Vindication of the Rights of Women* ilipochapishwa. Tangu hapo ufeministi umepitia mikondo tofauti tofauti. Mkondo wa kwanza wa ufeministi (karne ya 19-20) ulinua

kupinga maonevu dhidi ya mwanamke kwa kutetea haki ya mwanamke kisiasa. Mkondo wa pili kati ya (1960-1980) ulinua kupinga ubaguzi wa mwanamke kijamii na kitamaduni, kaida za kijinsia zilizomkandamiza mwanamke na kutetea jukumu la wanawake katika jamii. Mkondo wa tatu ulizuka miaka ya (1990-2000) kutokana na upungufu wa mkondo wa pili na ili kushughulikia aina za ufeministi zilizoibuka.

Showalter (1977) pia anadai kuwa uhakiki wa kifeministi hutofautiana na misimamo ya sasa ya nadharia za uhakiki kwa kuwa haupati misingi yake ya kifasihi kutokana na mamlaka moja au katika matini takatifu. Uhakiki wa kifeministi unaaminiwa kuwa ulitokana na viini kadha kupitia usomi mpana wa fasihi za wanawake; kupitia mabadilishano baina ya wananadharia wa ufeministi katika masomo mengine, hasa historia, saikolojia, anthropolojia na kutoka udurusu na urejelezi wa nadharia ya fasihi yenyewe.

Ni katika mkondo wa tatu wa mabadiliko ndipo tunapata ufeministi wa Kiafrika japo hii haimaanishi kwamba ni sehemu ya mkondo huu wa tatu bali ni kwa kuwa mivutano ya rangi ya Kiafrika na utamaduni inajitokeza humu. Katika kongamano la African Diaspora Studies Institute katika Chuo Kikuu cha Howard mwaka wa 1979 na Chuo Kikuu cha Nairobi mwaka wa 1981, suala la haja ya kukuza nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika lilijadiliwa. Wakereketwa wa masuala haya ya ufeministi walijadili kwamba kulikuwa na haja ya kuwa na nadharia itakayojumuisha aina mbali mbali za udhalilishaji wa mwanamke katika maeneo ya ubaguzi wa rangi, jinsia na utamaduni kwa sababu tajriba za watu weusi kitamaduni na kwa njia yoyote ile ni tofauti na za wengine. Haya yalisisitizwa na maelezo ya Leslie (1984), kwamba kuna haja ya kukuza nadharia

itakayomwezesha mwanamke kujitazama katika muktadha wa uhalisia wa kijamii na kitamaduni anakojiendeleza. Sayed Sadek (2014) anasisitiza sababu ya kuzuka kwa dhana ya ufeministi wa Kiafrika. Kwamba, sababu dhana ufeministi ina maana hasi ya kimatilaba barani Afrika hata kwa waandishi wanawake na wakati mwingine kurejelewa kama laana, wahakiki waafrika wamekuza dhana kadhaa zinazoweza kutumiwa kiubadala kama ufeministi wa Kiafrika.

Japo ufeministi ulianza Uropa, umeweza kuenea kote ulimwenguni hadi kufika Afrika ambapo wanawake wanakabiliana sio tu na wanaume bali pia na tamaduni na desturi zilizopitwa na wakati. Tofauti na ufeministi wa Kimagharibi, ufeministi wa Kiafrika unaibuka kutokana na haja ya kumkomboa mwanamke kutokana na jamii inayotawaliwa na ubabedume. Utamaduni au desturi, rangi ya watu weusi, jinsia na umenke, masuala ya kijamii na kiuchumi na ya kijamii na kisiasa ni baadhi ya mambo yanayoshughulikiwa katika nadharia hii.

Strobel (1980) anaeleza kuwa aina mbali mbali za ufeministi ni muhimu katika kushughulikia masuala anuwai ya kijamii katika maeneo tofauti ya kijeografia. Maelezo yake yalichangia uamuzi wetu wa kuteua nadharia ya ufeministi wa Kiafrika kuyashughulikia masuala ya kifeministi katika mazingira ya Kiafrika. Mkondo huu unanua kudai utendewaji wa haki na nafasi zinazostahiliwa na wanawake katika jamii, sio kwa sababu ya huruma bali kwa kuhifadhi haki na hadhi yao kama binadamu.

Collins (2000) anaeleza kuwa haitoshi kuhakiki masuala yanayomkumba mwanamke kwa msingi wa jinsia pekee bali kuna mambo mengine kama dini, umri, kabila na uraia yanayoingiliana na jinsia. Wamitila (2002) anaeleza kuwa ufeministi ni msingi na nia ya



kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kisiasa na kiuchumi. Ufeministi hudadisi msimamo na itikadi za kiume, huangazia misimamo tawala na kuzishambulia dhana za kiume kama ubabedume.

Kwa hakika uhakiki wa kifeministi hunuia kudhihirisha tajriba za wanawake kupitia maandishi yao. Swaleh (2011) anaeleza kuwa uhakiki wa kifasihi wa kifeministi ni kilembwe cha mwito wa kifeministi ambao masuala yake makuu yalikuwa ya kumwezesha mwanamke kisiasa, kijamii na kiuchumi. Anasema kuwa ufeministi unabadilika na una vitapo vingi vinavyobadilika na kuongezeka. Ili kufikia katika maelezo timilifu ya ufeministi kinzani ni muhimu kufafanua ufeministi hasa kwa kujikita katika muktadha wa Kiafrika. Ufeministi wa Kiafrika ni tapo linalojikita katika misingi ya maadili ya kimapokeo ya Kiafrika na linashughulikia masuala ya kijinsia na mengine yanayohusiana nayo katika mazingira ya kijamii na kiitikadi ya Kiafrika. Juhudi zake zinachochewa na haja ya kumkomboa mwanamke mwafrika kutokana na ubaguzi wa kitamaduni na kidini.

Njogu na Chimera (1999) wanaeleza mihimili ya kimsingi ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika kama; Ufeministi wa Kiafrika ni jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali anayojipata mwanamke wa Kiafrika ili kumsaidia mtu yeyote kuelewa hali hiyo. Mtazamo wa ufeministi wa Kiafrika vile vile hujaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na ambao hawategemei wanaume ili kujitambulisha na ambao kisaikologia ni wanawake wanaojitambuaa na kujiamini wala wasiwe wanahisi kama wenye udhaifu kwa ajili ya umenke wao.

Nadharia hii inanuia kuleta usawa wa wanadamu kwa upande wa jinsia na utamaduni. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za binadamu na wala si za kimaumbile na za kijadi. Ni mtazamo unaokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake wa wanawake kama kundi kama kundi linalodhulumiwa. Lengo muhimu la nadharia hii ni kuvumbua na kuziweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume. Pia inanuia kuchunguza historia ya fasihi ya jadi ya kike na kuwamulika waandishi wa kike waliotambua hali za wanawake na ambao wanaweza kuchukuliwa kama vielelezo kwa wasomaji wao.

Njagi (2013) anasisitiza hali ya utamaduni wa Kiafrika ambao umenuia kumdhibiti mwanamke na basi kuiandama jinsia ya kike hadi na mwanamke Msenegali wa *Barua Ndefu Kama Hii* ya Mariama Ba. Kauli hii ilishawishi kufanya uchunguzi wetu kwa msingi wa nadharia inayoipa umuhimu muktadha wa Kiafrika. Maelezo ya Christian (1985) na ya Miller (1990), yanaafikiana na yale ya Mbatia (2001), Wamitila (2002), Bressler (2003) na Wafula na Njogu (2007) katika maelezo yao kwamba ufeministi wa Kiafrika ni tapo linalopigania haki za wanawake katika muktadha wake wa Kiafrika kwa kumweka mwanamke wa Kiafrika kati na kuzingatia kwamba anakumbwa na masuala yanayotokana na utamaduni wake. Ni katika kushughulikia masuala haya ya kifeministi ndiko kunazuka falsafa, mikabala na misimamo tofauti tofauti kuhusu ufeministi na baadhi ya hiyo huweza kukinzana.

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ilitokana na ufeministi wenyewe ili kuhakiki masuala ya ufeministi katika jamii yenye utamaduni wa Kiafrika. Madai ya nadharia hii ni ya

utambuzi wa uwezo wa wanawake, ukombozi wa wanawake na mwito wa kuwapa wanawake nafasi sawa na wanaume katika nyanja za kijamii, kisiasa, kielimu, kiuchumi na kidini katika muktadha wa jamii inayotawaliwa na ubabedume. Christian (1985) anatambulisha kwamba kipengele muhimu kinachotofautisha ufeministi wa kiafrika ni ule uwasilishaji ung'amuzi wa kibinafsi wa mwanamke wa Kiafrika ambaye anachukua hatua kuu ya kujikomboa. Miller (1990) akitofautisha ufeministi wa Kiafrika na wa Kimagharibi anasema kwamba ufeministi wa Kiafrika huchunguza masuala ya kijinsia kwa mtazamo wa Kiafrika na kuchanganua nafasi ya mwanamke wa Kiafrika katika maeneo ya kijamii, kitamaduni na kiuchumi na kutathmini jinsi maeneo haya yanamdhalilisha mwanamke.

Kwa sababu hii tutayashughulikia masuala haya kwa mkabala wa nadharia ya ufeministi wa kiafrika unaodai kumtetea na kumkomboa mwanamke kutokana na mfumo wa kijamii unaodhibitiwa na ubabedume na kwa kuwa unajikita katika uelewa wa undani wa muktadha ya mwanamke wa kiafrika. Ufeministi katika muktadha wa Kiafrika hukabiliwa na utetezi wa haki na nafasi ya mwanamke; ukinuia kumkomboa mwanamke kutokana na asasi dhalilifu za kitamaduni zinazodhibitiwa na itikadi za kiume na kumpa mwanamke nafasi ya kuchangia katika jamii Bressler (2003).

Kwa mujibu wa Maduka (2005) ufeministi wa kiafrika haipingani na wanaume bali huwapa nafasi na hutilia maanani familia kama asasi ya jamii na wakati ule ule kumtetea mwanamke na nafasi yake pamoja na kukashifu itikadi zozote zinazomkandamiza mwanamke. Kwa hakika, ufeministi wa kiafrika ni kama ufeministi ulionasibishwa. Naye Steady (1981) anaeleza kwamba ufeministi wa Kiafrika unajumuisha ubaguzi wa rangi,

jinsia,na wa kitamaduni ili kuibua aina ya ufeministi ambayo ni jumuishiki zaidi na ambayo kwa kuipitia, wanawake hutazamwa kwanza kabisa kama binadamu wala si viumbe wa ashiki.

Davies (1987) ameangazia sifa sita za ufeministi wa Kiafrika; tutadondoa sifa tatu ambazo ni muhimu katika utafiti wetu kama; ufeministi wa kiafrika huchanganua elementi chanya za jamii za kiafrika kama ndoa za mitaala na jamaa hasa kuhusiana na uwajibikaji katika ulezi na ugawaji wa majukumu ya unyumba. Hata hivyo anaonyesha kuwa hali hii iligeuzwa na wakoloni na hadi sasa imegeuzwa. Pili, ufeministi wa kiafrika hujikita katika kuleta mwamko wa wanawake na wanaume kuhusiana na unyanyasaji na mizizi yake.

Tatu, ufeministi huu huchambua jamii za kiafrika ili kupata asasi ambazo ni za maana kwa wanawake na kutupilia mbali zile ambazo zinamdunisha na haiingizi ajenda za wanawake wa kimagharibi tu. Hatimaye, ufeministi wa kiafrika huenzi hali ya mwanamke wa kiafrika kujitegemea, kupenda ushirika, na kwamba kwa mwanamke mwafrika si kawaida kuajiriwa lakini huafiki kwamba kazi inayoleta riziki ni jambo lenye udhabiti. Mawazo haya ya Davies yana uhusiano na kazi tutakayofanyia uchunguzi. Kwa hivyo ni msingi muhimu tutakaoweza kujikita katika kuchambua na kuhakiki nafasi, majukumu na mitagusano ya wanawake kwa nia ya kuweza kuonyesha ukinzani uliopo. Ni katika mwanga huu ndipo tuliweza kuhakiki masuala ya kifeministi kwa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika.

### **1.8.2 NADHARIA YA ULINGANIFU AMILIFU**

Ulinganifu ni suala la kimsingi katika tafsiri na ulinganisho wa matini za lugha tofauti huhitaji nadharia ya ulinganifu. Ujumbe unapohawilishwa kutoka LC hadi LL mtafsiri anajihusisha na tamaduni mbili tofauti kwa wakati mmoja. Nadharia ya ulinganifu inatokana na ulinganifu ulioasisiwa na Catford (1965) na kuendelezwa na Nida na Taber (1969) Newmark (1988) na Pym (1993); wote wakikubali kwamba nia ya tafsiri ni kuibua matini ya LL ambayo ni sawa na ya LC.

Ulinganifu unaozungumziwa hapa ni ule unaozingatia uhusiano wa mpokezi na matini ambapo inaaminika kwamba uhusiano baina ya wapokezi wa lugha lengwa na matini ya lugha lengwa unafaa kulingana na uhusiano baina ya wapokezi wa lugha chanzi na matini ya lugha chanzi. Kuhusu utamaduni, ulinganifu amilifu unashikilia kwamba shughuli ya tafsiri inafaa kuchukua muwala wa kiutamaduni sawa na wa wapokezi lengwa. Kwa kuwa nadharia hii inazingatia sana hisia za wapokezi kuliko miundo ya lugha na kutilia maanani utamaduni wa lugha lengwa hupunguza uwezekano wa matatizo ya tafsiri yanayotokana na miundo tofauti ya lugha. Uhakiki wa tafsiri kupitia mwelekeo huu uliweza kutusaidia kufanya uchunguzi na kutoa mahitimisho yanayofaa.

Tuliongozwa na mihimili mitatu ya nadharia hii kama ilivyochangiwa na Zhang (2015) akiibua mawazo ya Bussmann (1996, 2000), Theodore Savory (1968) na Nida (1993);

- i) Ulinganifu wa kisemantiki; huu ulinganifu ni muhimu sana katika tafsiri zinazovuka mipaka ya tamaduni. Mhimili huu unahakikisha kwamba semantiki ya lugha chanzi inafikishwa katika lugha lengwa. Ni muhimu basi

kwa mtafsiri kuhakikisha kwamba uelewa wake wa matini unakaribiana sana na kile ambacho mtafsiri alinua kuwasilisha kwa wasomi wake.

- ii) Ulinganifu wa kimtindo; ulinganifu huu unahusu athari za kiulinganifu kuhawilishwa hadi lugha lengwa. Mtindo ni ule upekee unaomtambulisha msanii na kutambulisha hata hisia zake kwa wakati huo.
- iii) Ulinganifu wa kitamaduni; Ulinganifu huu unanua kuleta ulinganifu wa athari za kitamaduni baina ya hadhira ya tamaduni chanzi na hadhira ya tamaduni lengwa. Mhimili huu ndio muhimu zaidi kwa mihili yote ya nadharia ya ulinganifu.

Nida na Taber (1969) wanaeleza kuwa tafsiri ni mhimili ambao kwa kuupitia mtafsiri hutafuta kuamsha katika hadhira ya ML hisia kama katika hadhira ya MC na hutaka mpokeaji apate sio tu ujumbe bali pia mawazo, itikadi na falsafa za lugha ya kwanza. Tulishughulikia masuala ya uhawilishaji wa maana kwa mkabala wa nadharia ya ulinganifu amilifu tukizingatia kwamba mtafsiri hutafsiri kwa nia ya kumfikishia mpokeaji mawazo, itikadi na falsafa za LC.

Zaja (2006) akichunguza utathmini wa kinadharia wa fasihi tafsiri ya Kiswahili, anadai kwamba lengo kuu la uchunguzi wa fasihi tafsiri ni kudhihirisha uhawilishaji wa ulinganifu wa kanuni za kimuundo na kiisimu hata hivyo, anaeleza kwamba matini tafsiri huweza kusomwa, kufafanuliwa au hata kutolewa nadharia kwa misingi iliyo nje ya mifumo na miundo ya urasmi. Maelezo haya yalihalalisha uamuzi wetu wa kuteua nadharia ya ulinganifu katika tafsiri.

Kauli hii ina umuhimu kwa utafiti wetu kwa kuwa unajikita katika uhawilishaji wa maana wenye ulinganifu amilifu wa tafsiri bila ya kutarajia ulinganifu wa kimuundo au kiisimu. Akiendelea, anasema kuwa yapo mambo mengine yanayochangia MC kufikia HL kama ya kimatini, kimuktadha, kitamaduni na ya ufundishaji. Kauli yake ilichangia uchunguzi wetu kwamba katika uchunguzi wa uhawilishaji wa maana ya MC hatuwezi kupuuzwa muktadha wa kitamaduni ikiwa tutataka kuhitimisha kwamba matarajio ya HL yamefikwa.

### **1.9 MBINU ZA UTAFITI**

Mbinu hizi zinajumuisha njia zote za uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data na uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Kimsingi, uchunguzi wetu ulikuwa wa maktabani. Kwanza, tuliteua sampuli yetu; sampuli yetu ilikuwa matini lengwa ya tafsiri kwa kuwa itatupa mambo mahususi na ya kimsingi tu ambayo yanahitajika katika utafiti wetu. Tuliteua riwaya ya Ba, Mariama ya *So Long A Letter* na tafsiri yake ya *Barua Ndefu Kama Hii* kama iliyotafsiriwa na Clement Maganga. Baada ya kuteua riwaya hii tuliisoma na kudondoa masuala ya ufeministi hasa yaliyo na ukinzani na kuyaorodhesha. Tulidondoa pia hali na miktadha mbali mbali za mahusiano ya wahusika huku tukibainisha masuala ya kifeministi yanayoibuka kutokana nayo. Pia, tulidurusu kiuhakiki matini kadha zenye manufaa kwa utafiti wetu; zile zinazozungumzia masuala ya kifeministi na nadharia ya ufeministi wa Kiafrika na ulinganifu amilifu katika tafsiri zilizoko maktabani mwa vyuo. Tulisoma majarida na tasnifu zinazojadili maswala mbalimbali ya tafsiri na ya ufeministi pamoja na zile zinazozungumzia nadharia tulizotuea. Tulifanya hivi ili kukuza ujuzi wetu wa kiusomi na wa kinadharia ili kujenga

msingi wa kinadharia itakayotuongoza kufanya uhakiki. Tulisoma vitabu, majarida, na makala yaliyochapishwa na kutafuta mtandaoni kuhusu kazi zinazoshughulikia masuala ya ufeministi, mahusiano ya wahusika huku tukidondoa masuala yenyewe na kuyaorodhesha na hata zile zinazozungumzia nadharia tulizoteua.

Ukusanyaji wetu wa data ulifanywa kwa kuzisoma riwaya zote mbili na kuwapanga wahusika katika makundi kutegemea uhusiano, mitagusano, hadhi na miktadha yao mbalimbali na kuwaainisha kama; wake wa kwanza na wanawake wengine wanaowaunga mkono kwa upande mmoja, kisha wake wenza wao, wakwe zao wa kike pamoja na waume wao na ndugu zao na viongozi wa kidini kwa upande mwingine. Baada ya kuwapanga wahusika, tulidondoa na kuorodhesha baadhi ya masuala ya kifeministi yaliyowasilishwa katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* ili kuyatumia kuchunguza nafasi, misimamo na hata maamuzi yao kuhusu masuala hayo ya ufeministi. Hatimaye tuliorodhesha mahusiano baina na miongoni mwa wahusika huku tukionyesha masuala ya kifeministi yanayoibuka kutokana nayo kama vile suala la ulezi, usasa na ukale wa ndoa, usasa na ukale wa elimu, ushirikishwaji wa wanaume katika ufeministi, suala la unyumba n.k.

Tulichanganua data iliyokusanywa kimaelezo na kuifafanua kulingana na malengo ya utafiti na kuonyesha jinsi masuala hayo ya ufeministi yanahawilishwa hadi fasihi ya Kiswahili kwa kuegemea nadharia ya ulinganifu amilifu. Uchanganuzi wetu ulifanywa kwa kujadili na kutoa ithibati kutoka riwayani. Baada ya kuchanganua na kufafanua data tuliwasilisha matokeo kwa njia ya maelezo na kutoa mapendekezo yetu.



## **1.10 HITIMISHO**

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na msingi wa nadharia ambazo ni mbili; nadharia ya ufeministi wa Kiafrika na nadharia ya ulinganifu amilifu na mwishowe tukabainisha mbinu tutakazozitumia katika utafiti wetu

## **SURA YA PILI**

### **MAWASILISHO KINZANI YA MUSUALA YANAYOWAHUSU WANAWAKE**

#### **2.0 UTANGULIZI**

Wahusika ni viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na wasanii ili msanii awatumie kama sauti ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira anayoilenga. Katika kazi za kihalisia wahusika huwa vielelezo wa binadamu wa ulimwengu halisi ingawa si lazima sifa zao zote zifungamane na zile za binadamu wa ulimwengu halisia. Kimsingi, wahusika huainishwa kama wakuu au wasaidizi kutegemea wadhifa wao katika kazi husika na kuchunguzwa kwa kuainisha sifa zao na uhusika wao. Hata hivyo uchunguzi wa wahusika unaweza kufanywa kwa kuangazia mahusiano yao na wahusika wengine, majukumu yao ya kijamii na nafasi zao.

Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* imeandikwa kama barua kutoka kwa Ramatulayi kwa rafiki yake wa tangu utotoni; Aisatu katika muktadha wa Kisenegali baada ya utawala wa ukoloni wa Kifaransa. Riwaya hii ni hadithi ya safari ya mwanamke katike muktadha wa jamii ya Kisenegali unaobadilika. Riwaya hii inaweka sambamba hadithi za wanawake wawili wanaokumbwa na mapambano tofauti katika muda huu wa mpito ili kujitambulisha na ukombuzi waliopata na majukumu yao kama wake na kama walezi. Riwaya yenyewe imegawika katika visehemu vitatu ambapo sehemu ya kwanza; sura ya kwanza hadi ya tano mhusika mkuu, Ramatulayi anamweleza rafikiye wa utotoni, Aisatu kwamba amefiwa na mumewe Modu Falli. Hii inamtoa Ramatulayi kutoka hadhi ya kuwa mke na kumingiza katika ujane. Anazidi kumweleza rafikiye shughuli zote za matanga na mazishi yaliyofuata tukio hili la kufa kwa Modu.

Sehemu ya pili inaanzia sura ya sita hadi ya kumi na sita na inaangazia matukio ya zamani. Ramatulayi anakumbuka elimu ya kikoloni ya Kifaransa waliyopata na rafikiye kisha kuhusu ndoa zao na kukumbuka utengano wao na waume wao. Sehemu ya tatu inaanzia sura ya kumi na saba hadi ya ishirini na saba. Sehemu hii inaangazia maamuzi na uteuzi wa Ramatulayi kama mjane na kama mlezi wa pekee. Katika riwaya hii wahusika wanaume kama vile Modu Falli na Maudu Ba wamehusika. Modu Falli amehitimu uanasheria kule Ufaransa, Maudu Ba amehitimu kutoka shule ya udaktari ya Afrika. Tunaelezwa pia kuhusu maendeleo ya uanasheria ya Ibrahima Salli; mchumba wake Aisatu mdogo. Ni katika utawa wake wa siku arobaini ndipo Ramatulayi anawazia hali yake na yote yaliyompata. Hii inamchochea Ramatoulayi kueleza kuhusu mateso aliyopata, akihalalisha maamuzi yake, kumweleza matamano yote na kudhihirisha ukuruba wa hali zilizowapata. Barua hii ni kama njia ambayo kupitia kwayo anapunguza uzito wake wa moyoni.

Masuala yanayowahusu wanawake yamewasilishwa kwa uchangamano. Kimsingi, masuala haya ni ya kifeministi. Masuala haya yanachukua nafasi kubwa katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* na yamewasilishwa kwa uchangamano mkubwa kutokana na migongano ya kimahusiano, kiuteuzi, maamuzi na mitazamo ya wahusika. Masuala haya ya ufeministi yanazungukia masuala ya utamaduni na usasa wa elimu, unyumba, usasa na ukale wa ndoa., mpito na mvutano wa vizazi, wajibu wa wanandoa katika ulezi, uhuru wa kiuchumi na utegemezi wa kiuchumi na suala la uhuru.

## 2.1 UTAMADUNI NA USASA WA ELIMU

Kimsingi, katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* athari za elimu za aina tofauti zinazomwinua na kumponza mwanamke zinaangaziwa. Kwa jinsi suala la elimu limeangaziwa, wahusika wamegawika katika vikundi viwili. Kwa upande mmoja tuna Ramatulayi na Aisatu. Hawa wanawakilisha elimu ya kimagharibi. Kwa upande mwingine kuna Nabu Mdogo na Binetuu. Ramatulayi na Aisatu wanapata elimu ya kisasa inayonuiwa kuwainua kutoka utamaduni, ushirikina na desturi zinazomdhibiti mwanamke. Wawili hawa wamesoma na kuhitimu; Ramatulayi ni mwalimu katika shule ya upili huku Aisatu akiendelea masomo yake hadi kupata kazi katika ubalizi wa Ufaransa huko Marekani. Ramatulayi anaeleza;

Uwezo uliomo kwenye vitabu, vilivyogunduliwa kiajabuajabu na akili timamu ya binadamu unashangaza...vilikuruhusu kujikakamua. Yale ambayo jamii ilikunyima, vitabu vikakupa: baada ya kufaulu mitihani yako, nawe pia vitabu vikakupeleka Ufaransa (Uk. 61)

*The power of books, this marvelous invention of astute human intelligence....they enabled you to better yourself. What society refused you, they granted: examinations sat and passed took you also to France (Pg. 33)*

Elimu wanayopata Ramatulayi and Aisatu inawainua na kuwakomboa. Ni elimu ndiyo inayompa Aisatu uwezo wa kuacha ndoa inayomdhalilisha, kuanza maisha mpya na kujitegemea. Hata ingawa mivutano ya utamaduni ilishamiri, wawili hawa wanakumbatia usasa wa elimu na kujitenga na utamaduni ambao unaendeleza udhalilishaji na udhibiti na wanawake. Elimu ya kisasa inampa Aisatu uwezo wa kutosheleza mahitaji yake na hata kumwinua rafikiye kwa kumnunulia gari. Kwa maelezo yake Ramatulayi;

Sitasahau kamwe jamala uliyonifanyia wewe, dada yangu. Wala sitasahau kamwe furaha na mshangao nilioupata wakati ambapo muuzaji wa magari

ya aina ya Fiat aliponiita na kuniambia nichague gari nililotaka na kwamba wewe umegharamia kila kitu (Uk. 97)

*I shall never forget your response, you, my sister nor my joy and my surprise when I was called to the Fiat agency and was told to choose a car which you had paid for (Pg.56).*

Katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*, Ramatulayi anakumbuka tetesi za hasira zilizoenea baada ya Aisatu kuolewa na daktari kutoka tabaka la juu; Maudu Ba. Ilienea kwamba wasichana wamepotosha na elimu kasha wao huja kuwapotosha wanaume. Ikasemwa;

‘Shule inawageuza mabinti zetu kuwa mashetani wanaowapotosha wanaume.’ (Uk. 36)

*‘School turns our girls into devils who lure our men away from the right path.’ (Pg. 17)*

Nabu anatomia uwezo wake kumshawishi mwanawe aliyeelimika; Maudu Ba kuoia mke wa pili aliyemteua mwenyewe kwa hivyo anavunja ndoa ya kwanza ya mwanawe inayojikita katika mapenzi na maafikiano ya kiusomi. Ana mtazamo finyu kuhusu mfumo wa kitabaka na elimu rasmi ya viwango vya juu kwa mwanamke. Anamaka;

Nami najiuliza jinsi gani mwanamke anaweza kujijengea maisha yake kwa kupiga domo tu tangu asubuhi hadi jioni. (Uk. 57-58)

*In fact, I wonder how a woman can earn a living by talking from morning to night. (Pg. 30)*

Kwa upande mwingine, Nabu mdogo anakuzwa na kulelewa chini uangalifu wa shangazi yake. Shangazi yake anatahadhari sana Nabu mdogo asije akaathiriwa na usasa; usasa huu ni ule unaoletwa na elimu ya kisasa. Anahakikisha kwamba Nabu mdogo amepata elimu ya kisasa lakini kwa viwango ambavyo havingeweza kumpa uhuru wa kupindukia au kumfanya ajitenge na utamaduni. Kwa sababu hii, alimlea Nabu mdogo akimfunza

kupitia hadithi za fasihi ya kale hadi maadili yakajikita katika mtoto huyu. Tokeo lake ni kumwandaa mwanamke aliyepata kiwango kilichokadiriwa cha elimu kisha kufinyangwa kwa mafunzo ya fasihi ya kale yaliyojaa maadili. Inaelezwa;

Athari ya shule haikuwa kubwa kwa Nabou mdogo kwa vile Shangazi Nabou alihakikisha kwamba katika kutimiza lengo lake la kulipiza kisasi ilibidi amwandae huyo binti kwa namna ambayo ingalilingana na shabaha zake na wala hakutoa nafasi kwa athari nyingine yoyote. (Uk.85)

*School had not left a strong mark on young Nabou, preceeded and dominated as it was by the strength and character of Aunty Nabou who in her rage for vengeance had left nothing to chance in the education she gave her niece (Pg. 49)*

Ramatulayi na Aisatu wanatambua faida za elimu ya kisasa inayowakomboa, kuwapa uhuru na kuwawezesha kujitegemea. Wanaikumbatia elimu hii na kuacha ukale. Binetuu anaruhusu mataminio ya mamake ya maisha mazuri kumfanya awache ndoto zake za elimu na kujiingiza katika ndoa, asiyoipenda; ndoa ambayo ilimfisha akiwa hai. Ramatulayi anaeleza;

Bibi Mama-mkwe akalia sana. Na Binetuu je? Hakujali chochote. Angefanya nini na yote yaliyokwisha semwa yalikuwa kweli tupu. Moyoni mwake tayari alikuwa amekwishakufa... tangu siku aliposherehekea kuolewa kwake na Modu. (Uk. 127)

*Lady Mother-in-Law sobbed. Binetou? Indifference itself. What did it matter to her what was being said? She was already dead inside...ever since her marriage to Modou. (Pg. 74)*

Huenda angeendeleza masomo yake angefika upeo wa juu wa elimu na hata labda kumpata mume anayemfaa. Binetuu anakumbatia utamaduni na ukale unaotambulisha utamaduni huo na kuuacha usasa. Hali ya ukinzani inaibuka kutokana na elimu ya kisasa kusawiriwa kama chombo cha kumkomboa, kumwinua na kumpa mwanamke uhuru na kwa upande mwingine kusawiriwa kwa elimu ya kale kama chombo kinachomyima

mwanamke uhuru, kumponza na kumdhibiti mwanamke kiasi cha kumfanya asijitambue kibinafsi. Pamoja na haya, kumesawiriwa wanawake ambao wanaegemea pande zote mbili. Isitoshe, ukinzani anaibuka tunapowaona baadhi ya wanawake wakikumbatia utamaduni na ukale uliomo na kujitenga na elimu ya kisasa inayofaa kumwinua.

## **2.2 SUALA LA UNYUMBA**

Masuala ya unyumba kimsingi huwa yanahusishwa na wanawake. Katika jamii ambayo inakumbwa na mpito wa wakati na mivutano ya ukale na usasa inayoletwa na mpito huu husababisha suala la unyumba kuchukua sura tofauti. Hali hii inajitokeza katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Mhusika mkuu Ramatulayi ana wahudumu wawili wa nyumbani na mawifi zake wanadhani anawalimbikizia watu wengine majukumu ya nyumbani. Hata hivyo, anahakikisha kwamba shughuli zote za unyumba zimetimizwa hata wakati mwingine kuingilia shughuli zenyewe na kuzifanya mwenyewe. Ramatulayi anapaswa kuwajibikia masuala haya ya unyumba ipasavyo hata ingawa afikapo nyumbani kutoka kazini huwa amchoka.

Mwanamke ambaye anafanya kazi huwa na majukumu mawili makuu ambayo lazima ayawajibikie kwa usawa. Ramatulayi anafaidika kutokana na hali hii yake ya maisha kwani inamwezesha kuishi kwa starehe na kumiliki vifaa vingi anavyovimudu kutokana na na juhudi zake mwenyewe. Haya yanaibuka katika jamii inayoamini kwamba shughuli za unyumba ni za wanawake pekee. Hata ingawa amelimika, analazimika kuwajibikia kikamilifu wajibu wake wa unyumba kama inavyoafikiana na utamaduni wa jamii. Tofauti ni jinsi ambavyo Daba na bwanake, Abu wanavyosaidiana katika kazi za

unyumba. Mumewe anamsaidia kufanya kazi ambazo kitamaduni zinatazamwa kama za mwanamke. Huu ni usasa unaojitokeza katika suala la unyumba.

Ramatulayi anatambua umuhimu wa wale wanawake wanaoitwa kina mama wa nyumbani. Anatambua mchango wao katika kuitunza nyumba. Anatambua mchango wao katika kuitunza nyumba na kudhibiti bajeti ya familia. Tunapochunguza usawiri huu, kwamba ameelimika na kwa hivyo kutarajiwa kwamba usasa umekolea kwake, mtazamo wa Ramatulayi kuhusu suala la unyumba unakuwa kama suluhu ya mivutano ya ukale na usasa.

Mtazamo wake Ramatulayi unakinzana na wa wafi zake ambao hawamwonei wivu kwa hali yake ya maisha kwa kuwa wanamwona anavyojishughulisha baada ya kazi nzito shuleni. Wao wanafurahia starehe zao, utulivu wao na nyakati zao za kujistarehe. Wanakubali kutunzwa na waume wao ambao wamekalifishwa na majukumu yao. Wanawake hawa wamekabidhi uhuru wao mikononi mwa waume wao na kijinyima uhuru wa kiuchumi. Ramatulayi anaeleza;

Some of my sisters-in-law did not envy my way of living at all. They saw me dashing around the house after a hard day in school. They appreciated their comfort, their peace of mind, their moments of leisure and allowed themselves to be looked after by their husbands, who were crushed under their duties. (Pg. 20)

*Baadhi ya mawifi zangu hawakuionea wivuhali ya maisha niliyokuwa nayo. Waliniona nikihangaika nyumbani baada ya kazi nzito huko shuleni. Walifurahia starehe yao na utulivu wao, na nyakati zao za mapumziko, na walipendelea kustareheshwa na waume zao waliolemewa na mizigo mikubwa. (Uk. 41)*



## 2.3 USASA NA UKALE WA NDOA

Riwaya ya Mariama Ba inawasilisha suala la ndoa hivi kwamba wahusika waliomo wanawakilisha hali zote za wakati; usasa na ukale kwa mpigo. Modu Falli amesawiriwa kama aliyepewa nguvu kidini na kitamaduni katika asasi ya ndoa juu ya wake zake. Wake zake wanawakilisha usasa na ukale wa ndoa kwa wakati mmoja. Ramatulayi mkewe wa kwanza anawakilisha hali ya ukale na ndoa. Ni mkewe wa kwanza kwa hivyo utamaduni unamlazimu kumtii na kufuata maamuzi ya mumewe. Hata hivyo baada ya Modu kuoja mke wa pili, Ramatulayi anatambua kwamba amedhalilishwa na kunyimwa uhuru kwa muda mrefu na hivyo usasa unaanza kuingia kupitia kwa ujitambuzi na kibinafsi na ni katika tamko hili lake ndiko hali hii inadhihirika;

My voice has known thirty years of silence, thirty years of harassment. It bursts out, violent, sometimes sarcastic, sometimes contemptuous. (Pg. 60)

*Sauti yangu ilijua miaka thelathini ya kukaa kimya na miaka thelathini ya kazi ngumu. Ikalipuka na ukali, ama wa kejeli au wa dharau. (Uk.103)*

Binetuu anadhihirika kama kiwakilishi cha usasa wa ndoa kwa kiwango kidogo na ukale wa ndoa kwa kiwango kikubwa. Anapendelea kutumia pesa za bwanake kwa vitu kama magari, vileo na kujistarehesha vilabuni. Hata hivyo, amefungwa na hali ya ukale kwani anapofiwa na mumewe anashindwa kujitambua kibinafsi kama mwanamke na kubaki na tatizo la kujitambua kibinafsi kwa sababu mwanamke wa kale anatambulika akiwa na mume wake.

Ramatulaye na Aisatu wanawakilisha wanawake wa Afrika mpya kwani wameelimika. Hata hivyo, wanakua katika jamii yenye mivutano ya kidini kifamilia kitamaduni na ya mpito wa wakati. Ndoa yake Ramatulayi ilisherehekewa bila ya mahari kama

inavyohitajika kitamaduni, na bila ya maandalizi ya sherehe kubwa ilivyotarajiwa. Hii inadhihirisha mpito kutoka utamaduni na kuingia kwa usasa wa ndoa ambapo mahari si lazima kutolewa. Kwa upande wake, Aisatu ameolewa na Maudu Ba daktari wa tabaka la juu naye alitoka tabaka la chini. Anapoulizwa, Maudu Ba alijibu kwamba ndoa ni uamuzi wa kibinafsi. Ndoa yao ni ishara ya uvunyaji na vidhibiti vya ndoa vinavyowekwa na utamaduni na ukale na kuingia kwa usasa wa ndoa.

Baada ya kutelekezwa na mumewe, Ramatulayi anafanya uamuzi na kubaki katika ndoa yao. Kwa kufanya hivi anadhihirisha msimamo tofauti na Aisatu na kutambua haki zake kama mwanamke huru katika ndoa. Ni mfano na mwanamke anayeamua kubaki kwenye mipaka ya kijamii na kutaka kuendeleza ujitambuzi wake kibinafsi bila ya kukiuka utamaduni. Anasema;

Mimi ni miongoni mwa wale kina mama ambao hawawezi kuonyesha uwezo wao wa kujikakamua isipokuwa tu katika ndoa. (Uk. 100)

*I am one of those who can realize themselves fully and bloom only when they form part of a couple. (Pg. 58)*

Aisatu kwa upande mwingine anawakilisha usasa wa ndoa kwa kufanya uamuzi na kumtaliki mumewe. Anadhihirisha utambulizi wa haki zake kama mwanamke huru nje ya ndoa na hata kukwea ngazi ya kikazi akiwa nje ya ndoa. Aisatu ni kielelezo cha mwanamke anayeamua kuvunja mipaka ya kijamii inayowadhibiti wanawake na kuporomosha mfumo wa kibabedume. Wawili hawa wanaelewana kwa kuwa wote wana tajriba sawa na wote ni waathiriwa wa ndoa za mitaala. Tofauti baina yao inajitokeleza katika misimamo yao tofauti kuhusu hatua za waume wao kuo wake wa pili. Ramatulaye anaamini kwamba wanawake wanapaswa kujikomboa lakini pia anazingatia

maadili ya ukale ya kiafrika yasiyoafikiana na mihimili ya ufeministi. Aisatu anadhihirika kama mwathiriwa asiyetarajiwa wa maisha na pia kama mwanzilishi jasiri wa miasha mapya. Kwa kifupi, riwaya hii imesawiri kikundi kimoja cha wanawake wanaojaribu kuendeleza shughuli zao katika ndoa kwenye jamii yenye ubabedume huku kikundi kingine kinajaribu kujiendeleza kibinafsi nje ya ndoa na utamaduni.

#### **2.4 MPITO NA MVUTANO WA VIZAZI**

Kihalisia, mabadiliko yanayoletwa na usasa ndio chanzo cha mpito wa vizazi. Mivutano ya vizazi nayo hushurutishwa na utamaduni na ukale kwa upande mmoja na usasa kwa upande mwingine. Mivutano ya vizazi inashurutishwa na utamaduni na ukale. Kwa upande mmoja na usasa kwa upande mwingine. Katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* kunasawiriwa vizazi vitatu. Kizazi cha kwanza cha mama zao Aisatu na Ramatulaye pamoja na mama mkwe zao. Kizazi cha pili ni pamoja Aisatu, Ramatulayi, Binetuu na Nabu mdogo. Kizazi cha tatu ni cha wanao. Kimsingi kunaibuka ulinganisho unaoibua tofauti za kizazi cha mama na cha binti yake na kuangazia mabadiliko katika ulimwengu ambayo yameletwa na jamii ya kisasa na ambayo yanasabasisha mivutano baina yao na mama mkwe zao.

Ni kutoka kizazi cha mama zao Ramatulayi na Aisatu ndiko kunajitokeza mpito wa vizazi. Hata hivyo mpito wenyewe hauji bila vikwazo kwa kuwa mabadiliko ya ulimwengu ya kutoka ukale na kuingia usasa yanaanzia katika kizazi cha Ramatulaye na Aisatu. Kwa sababu hii, wawili hawa wanajipata katika hali ya mtanziko kati ya ukale na mpito wa kuelekea usasa. Ukale unahusiana na utamaduni na ambao unamdhibiti mwanamke na kumpa nguvu mwanaume, unaomyima mwanamke uwezo na kujikomboa,

kumtaka mwanamke afuate maamuzi ya mwanaume na kunyima uhuru umeandama na na kukita mizizi yake katika kizazi cha pili.

Kihalisia, mabadiliko yanayoletwa na usasa ndio chanzo cha mpito. Binetuu na Nabu mdogo ni vielelezo vya wanawake wa kizazi cha pili ambao wanaendeleza desturi za kizazi cha kwanza. Hakuna mgongano unaojitokeza baina yao na kizazi cha kwanza. Ndio, wamelelewa katika jamii ambayo usasa unaingia lakini wanafungwa na ukale na utamaduni wa ndoa zao, kwa hivyo wanaendeleza usasa lakini usasa wenye mipaka kwani utamaduni hauwaruhusu kuwa na uhuru kamili.

Kufikia kwa kizazi cha tatu cha wanao Ramatulayi na Aisatu, tayari usasa umekita mizizi na watoto wao ni kielelezo cha kizazi cha tatu ambao wanakua katika mukadha wenye usasa. Usasa wao unajidhihirisha kupitia mavazi yao, uvutaji wa sigara na uhuru wao wa kutangamana na wavulana. Ni katika kizazi cha pili ndipo tunapata hali ya mvutano. Katika mivutano hii, ni Aisatu na hasa Ramatulayi ndio waathiriwa wakuu kwani wao ni kama daraja ya mpito wa vizazi. Kizazi cha tatu ni kielelezo cha mpito kamili wa vizazi kutoka kizazi cha kwanza. Kauli hii ya Ramatulayi inathibitisha haya;

Kizazi chetu kimebahatika kuwa kuingo cha enzi mbili tofauti, enzi ya ukandamizwaji na enzi ya uhuru. Tulikuwa bado vijana wakakamavu tulipokuwa tunatayarisha mipango ya kujipatia uhuru. (Uk. 49)

*It was the privilege of our generation to be the link between two periods in our history, one of domination, the other of independence. We remained young and efficient, for we were messengers of a new design. (Pg. 25)*

## **2.5 WAJIBU WA WANANDOA KATIKA ULEZI**

Majukumu ya ulezi yamebadikila kutoka vizazi vya awali hadi sasa. Mabadiliko haya yanajitokeza katika wanaowajibika katika ulezi na pia katika misingi ya ulezi, yaani ulezi

wa kikale au wa kisasa. Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* ni riwaya yenye uchangamano wa suala la ulezi. Zamani, ulezi ulikuwa wajibu wa jamii nzima. Watoto walilelewa na wanajamii na hata wanajamii walichukua zamu kuwalea watoto. Ramatulayi anakumbuka jinsi mama zao walivyobishana kuhusu atakayewatunza shangazi na wajomba wao. Jukumu la ulezi lilifanikishwa na ushirikiano wa wanajamii wote tofauti na wakati wao Ramatulayi na Aisatu.

Baada ya Aisatu kumtaliki mumewe na Ramatulayi kutelekezwa na mumewe. Wote wawili waliachiwa jukumu la ulezi wa wanao peke yao. Aisatu anachukua jukumu lote la kuwalea wanawe. Tunafahamu kwamba dini ya Kiislamu inampa mume uhuru na kuo wake wengi, dini hii pia inamtaka mwanaume amgawie mali mkewe wa kwanza na kuwajibikia jukumu la ulezi. Hata hivyo, katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*, Modu anamwacha Ramatulayi bila chochote na kumtwika mzigo wa ulezi na wanao kumi na wawili na kumsahau Ramatulayi na wanawe kabisa. Tukio hili linadhihirisha kwamba huku Modu anaegemea uhuru na kuo wake wengi anaopewa na dini. Hata hivyo, anapowatelekeza wanawe na mkewe anavunja baadhi ya kanuni za dini yenyewe zinazomhitaji kutekeleza wajibu wake kwa wanawe na mkewe na kumwoa Binetuu. Ramatulayi anawaza;

Je, Modu alishawahi kulipima pengo kubwa aliloliacha katika nyumba hii?  
Je, alikuwa amenipa nguvu zilizokuwa zaidi ya zile za kwangu ili niweze kuwasaidia wanangu wafanikiwe? (Uk. 96)

*Did Modou appreciate, in its full measure, the void created by his absence in this house? Did Modou attribute to me more energy than I had to shoulder the responsibility of my children? (Pg. 55)*

Je, nilikuwa na uwezo wa kuubeba peke yangu mzigo huo uliokuwa na wajibu wa kihali na kimaadili? (Uk. 73)

*Did I have enough energy to bear alone the weight of this responsibility, which was both moral and material (Pg. 41)*

## **2.6 USASA NA UKALE WA SUALA LA MALEZI**

Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* inawasilisha ulezi wa kisasa unaoendelezwa na Ramatulayi. Ulezi huu unadhihirika kupitia kwa mavazi ya wanawe, uvutaji sigara kwa wasichana, njia zake za kuwakosoa kitabia na uhuru anaowapa wanawe, wa kuenda sinema na kutangamana na wavulana. Hata hivyo, wakati anapokumbana na shida katika malezi ya wanawe Ramatoulayi hupata uelekezi kwa kurejelea mafunzo ya nyanyake. Mwelekeo wake aliochukua kuwaadhibu wanawe ni wa kisasa; wa kuwaelekeza, kuwatia moyo kuwahimiza na kuwapa nasaha badala ya kutumia vitisho. Msimamo wake kuhusu ulezi ulitofautiana na ule wa Farmata, wawili hawa wana mitazamo tafauti kuhusu ulezi. Farmata amekolezwa ukale na anaendelea kumpa Ramatulaye mitazamo yake akiamini ana jukumu kama mwanamke mkubwa katika tabaka la chini. Wakati Aisatu anapatikana kuwa mja mzito Farmata anajikita katika kumuonya na kumtishia mvulana aliyemtunga mimba Aisatu jambo ambalo Ramatulayi hakuhangaika nalo. Ramatulayi kwa upande wake halipi uzito suala la kosa lake Ibrahim. Analiona kama tatizo dogo anapowazia uwezekano wa masomo ya binti yake. Kwake, la umuhimu ni kuhakikisha bintiye hajakatiza masomo yake.

Ramatulayi na Aisatu wana tajriba sawa kwa kuwa wote wamekumbwa na matatizo ya ulezi. Tafauti baina yao ni kuwa Aisatu aliamua kuchukua jukumu la ulezi kwa kupenda hata ingawa Maudu aliendelea kutekeleza majukumu yake ilhali Ramatulayi analazimika kubeba mzigo huu za kuwalea wanawe peke yake baada ya kutekelezwa na mumewe. Aliwaza vipi angeweza kuwajibikia jukumu hili ambalo aliona kuna nzito kwani alipaswa

kuwalea akiwafunza maadili pamoja na kwamba malezi yao yalimtaka kukidhi mahitaji yao mengi. Ukinzani unajitokeza katika majukumu yaliyochukuliwa na waume wao katika ulezi. Ramatulayi anaelezea mawazo yake;

Wasiwasi wangu ulikuwa kwenye masuala mengine siyo yale ya Farmata. Tulikuwa katikati ya mwaka wa masomo. Nitafanyaje ili binti yangu asirudishwe nyumbani? (Uk. 152)

*My preoccupations were different from those of Farmata. We were right in the middle of school year. What was to be done to prevent my daughter's expulsion from school. (Pg. 90)*

## **2.7 SUALA LA UHURU**

Suala la uhuru linaibua uchangamano linapotazama kwa muktadha wa Kiafrika. Tukumbuke kwamba tunamaanisha uhuru kwa mwanamke katika muktadha unaomtaka mwanamke abaki chini ya udhibiti wa utamaduni na kumtaka aafikiane na maadili ya utamaduni wa Kiafrika na maadili ya utamaduni wa Kiafrika. Ni kwa mwanga huu ndipo tunaweza kuchanganua hali za uhuru na wahusika Ramatulayi, Aisatu, Binetuu na Nabu mdogo katika riwaya. Riwaya hii inawasilisha safari ya nchi ya Senegali kujikomboa kutoka ukoloni na safari ya wanawake kujikomboa sambamba na safari hiyo. Uchangamano wa suala la uhuru unajitokeza katika uhalisia uliopo riwayani. Kwa upande mmoja kuna wanawake wanaotaka kujiendeleza nje ya mipaka ya utamaduni na ukale na kutaka ujitambuzi wa kibinafsi kama wanawake. Wanawake hawa wanawakilishwa na Ramatulaye na Aisatu. Kwa upande mwingine kuna wanawake ambao wanakubali kubaki katika jamii yenye ubabedume, kudhibitiwa na utamaduni na kujiendeleza ndani ya mipaka ya utamaduni na kivuli cha ukale. Hali hizi mbili za uhuru zinakinzana. Uhuru wa mwanamke unatokea kama zao la uamuzi wake.

Ramatulaye na Aisatu wanawakilisha wanawake wanaotaka kuvunja mipaka ya utamaduni na kipata uhuru. Hata hivyo kuna tofauti baina ya uhuru wao. Ramatulaye anapotelekezwa na mumewe anabaki katika ndoa hiyo. Sababu ni kwamba alijihisi kama mmoja wa wale wasioweza kufanikiwa na kujiendeleza kikamilifu nje ya asasi ya ndoa. Uteuzi huu wake unamfanya asifikie upeo wa uhuru wake japo amelimika. Anasema;

Mimi ni miongoni mwa wale kina mama ambao hawawezi kuonyesha uwezo wao wa kujikakamua isipokuwa tu katika ndoa. (Uk. 100)

*I am one of those who can realize themselves fully and bloom only when they form part of a couple. (Pg. 58)*

Hata hivyo, anatambua kwamba kwa muda mrefu hajapata uhuru na tokea kutelekezwa na Modou, alijisaili na kupata uwezo wa kujitetea. Anaendelea;

My voice has known thirty years of silence, thirty years of harassment. It bursts out, violent, sometimes sarcastic, sometimes contemptuous. (Pg. 60)

*Sauti yangu ilijua miaka thelathini ya kukaa kimya na miaka thelathini ya kazi ngumu. Ikalipuka na ukali, ama wa kejeli au wa dharau. (Uk.103)*

Anatambua kwamba mfumo wa kijamii unampa nguvu mwanaume kuliko mwanamke lakini hana nia ya kuporomosha mfumo wenyewe bali anauia kujitambua na kujipa uhuru ndani ya mfumo huu wa kijamii. Mkabala wake ni ule wa kutafuta namna ya kijiendeleza bila kukiuka utamaduni kwa imani ya kuwa wakati utafika wa kubadili maisha yake. Hata ingawa anaona ugumu wa kujitenga na tamaduni na kanuni za dini ya Kiislamu, hajatamauka na anafahamu kwamba duniani kote kuna msukosuko wa mkondo wa kuwakomboa wanawake. Kwa hakika uteuzi wake unashinikizwa na mivutano ya kidini, kifamilia na kitamaduni kwa upande mmoja na usasa kwa upande mwingine. Hata hivyo anafurahia anapona mwanamke akishinda vidhibiti anavyowekewa na kujipa uhuru.



Anataka uhuru lakini anafahamu changamoto za mwanamke anayejisimamia peke yake katika jamii inayomtambua mwanamke anapokuwa na mume. Mawazo yake kuhusu uhutu wa mwanamke yanafumbatwa na kauli hizi zake;

Huku jamaa wakinishangilia, nilitathmini ufinyu wa uhuru aliopewa mwanamke. (Uk. 94)

*From the surprised looks, I gauged the slender liberty granted to women. (Pg. 54)*

Mapambano yasiyoweza kuzuilika yanayoubadili ulimwengu hivi sasa mintarafu ya uhuru wa mwanamke sitaki yanipite hivi hivi tu... Moyo wangu huchanua kila mara nimwonapo mwanamke anatokeza katika giza. (Uk. 158)

*I am not indifferent to the irreversible currents of women's liberation that are lashing the world... My heart rejoices each time a woman emerges from the shadows (Pg. 93)*

Kwa upande wake, baada ya Maudu Ba kumtaliki Aisatu na kumwoa mke na pili Aisatu anajitwika mzigo wa kuwalea wanawe na kuondoka. Anajitenga na ndoa ambayo haingempa furaha na kujiendeleza nje ya ndoa. Aisatu anaondoka na kujingiza katika masomo na vitabu vikawa tegemeo lake. Hatua hii ya Aisatu inampa uhuru wote nje ya utamaduni na mbali na dini inayompa nguvu mwanaume na kumdhibiti mwanamke. Hakujishughulisha tena na Maudu ambaye alikuwa chanzo cha madhila yake. Aisatu ni kielelezo cha upeo wa juu wa uhuru unaoandamana na usasa. Elimu yake Aisatu inampa njia ya kujiendeleza kwa kumpa nguvu za kiuchumi na kumfanya akasahau mateso aliyoyapitia na kufikia kilele cha maendeleo anapoishia kufanya kazi ubalozi wa Ufaransa huka Marekani. Haya yanathibitishwa na kauli hizi;

Na ukaondoka. Ulikuwa na ujasiri wa unaoshangaza kwa kuyakabili kikamilifu yale maafa yaliyokupata. Uwezo uliomo kwenye vitabu... Yale ambayo jamii ilikunyima, vitabu vikakupa: baada ya kufaulu mitihani yako, nawe pia vitabu vikakupeleka Ufaransa. (Uk. 61)

*And you left. You had the surprising courage to take your life into your hands... The power of books... What society refused you, they granted: examinations sat and passed took you also to France. (Pg. 33)*

Wala hukuwa na wasiwasi na Maudu. Kwa hakika ulikuwa pale, maafa uliyoyapitia umeyakanyaga chini ya kisigino chako. (Uk. 64)

*You did not care about Maudu. Yes, indeed, there you were, the past crushed beneath your heel. (Pg. 35)*

Aisatu alikabiliwa na vizingiti vya kidini na vya kitamaduni lakini aliweza kuvipiga vita na kuporomosha mfumo wa ubebedume. Alitishiwa kwamba hangeweza kujisimamia peke yake kama mwanamke. Akaambiwa kwamba wanawake wanahitaji ulezi wa baba yao, akahimizwa asiukate mkono unaomlisha lakini kwa haya yote hakuyaruhusu kumpotosha na njia aliyokwisha fuata. Hakuruhusu mivutano ya kidini na kitamaduni kumwekea vikwazo na kumweka katika hali ya mtanziko wa kujitenga na ukale na kukumbatia usasa au kuuafiki ukale pamoja na utamaduni uliopo. Usawiri wa uhuru wake Aisatu na wa Ramatulaye unafanya riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* kuwa kama suluhisho la mivutano baina ya dini na utamaduni kwa upande mmoja na usasa kwa upande mwingine.

## **2.8 SUALA LA UHURU WA KIUCHUMI NA UTEGEMEZI WA KIUCHUMI**

Suala la uhuru wa kiuchumi na utegemezi wa kiuchumi linaibuka kutokana na uchanganuzi wa Ramatulayi na Aisatu kwa upande mmoja na Bibi Mama- mkwe, Nabu mdogo na Binetuu kwa upande mwingine. Kwa sababu ya kuelimika, Ramatulayi na Aisatu wameweza kupata kazi. Mapato yao yamewawezesha kupata uhuru wa kiuchumi. Kwa upande wa Aisatu, uhuru wake unaotokana na kujitambua na kujikomboa kutokana na udhibiti wa mwanaume na hasa utamaduni ndio unampa uwezo wa kumtaliki mumewe

lakini uhuru wake wa kiuchumi ndio unampa uwezo wa kujiendeleza kimaisha, kimasomo na kukidhi mahitaji ya wanawe bila ya kumtegemea mumewe au mwanaume yeyote. Isitoshe, uhuru huu ndio unampa uwezo wa kumwauni rafikiye Ramatulayi kwa kumnunulia gari; hatua hii yake Aisatu ilimshangaza Modu.

Baada ya kutelekezwa na mumewe, Ramatulayi mwanzoni aliwaza vipi angewalea wanawe kumi na wawili. Anakiri kwamba maisha yalikuwa magumu baada ya kutelekezwa na Modou lakini anasisitiza kwa kauli hii ‘niliishi’ au ‘nikaweza kuishi’ jinsi alivyopambana hadi akaweza kujiendeleza. Mbali na majukumu yake alihitaji kutekeleza majukumu ya mumewe. Anasema;

Nikaweza kuishi. Licha ya mzigo niliokuwa nao tangu zamani, nikaubeba na ule uliokuwa wa Modu. (Uk. 93)

*I was surviving. In addition to my former duties, I took over Modou's as well. (Pg. 53)*

Hata hivyo, ingawa alikumbana na ugumu wa maisha mwanzoni, Ramatulayi aliweza kujiendeleza kiasi cha hata kuonewa wivu na baadhi ya mawifi zake; ambao walipendelea kustareheshwa na waume zao ambao tayari walikuwa wamelemewa na mizigo mikubwa.

Kwa upande wa Bibi Mama- mkwe na Binetuu, uhuru wao wa kiuchumi ulidhibitiwa kutokana na kuwepo chini ya mwanamume na kupendelea kumtegemea mwanaume. Binetuu aliweza kuendesha gari, kunywa vileo vya aina mbali mbali, kuvalia mavazi ya kifahari na kujibarizi katika vilabu vingi kwa sababu ya utajiri wa mumewe, kwa kuacha ndoto zake za masomo alikuwa anatoa uhuru wake wa kiuchumi mhanga ili mamake apate kudiriki maisha mazuri. Ukweli huu unajidhihirisha riwayani ifuatavyo;

Uhalisia huo ulikuwa Binetuu mwenyewe aliyetamba kutoka klabu moja ya usiku hadi nyingine. Alifika amevaa kanzu ndefu ya gharama, kiunoni kajifunga mkanda wa dhahabu... (Uk. 91)

*Reality was also Binetou who went from night club to night club. She would arrive draped in a long costly garment, a gold belt... (Pg. 52)*

Binetou alikuwa mwana kondoo aliyetolewa kama sadaka kwenye madhabahu ya mali... (Uk. 72)

*Binetou, like many others, was a lamb slaughtered on the altar of affluence... (Pg. 41)*

Bibi Mama-mkwe anamshinikiza Binetuu akatize masomo yake ili aolewe na Modou kwa kutaka kupandisha hadhi yake katika jamii na kupata utajiri alioutamani. Hata hivyo hadhi yake na utajiri ulididimia wakati Modou alipofariki. Kwa kila hali, uchanganuzi wa uhuru wa kiuchumi wa wahusika hawa kunaibua hali mbili kinzani.

## **2.9 HITIMISHO**

Kwa muhtasari, utafiti wetu ulilenga kuchunguza uelewa unaoibuliwa na masuala ya kifeministi katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* kwa kujikita katika mihimili ya nadharia ya ufeministi kinzani na ya ulinganifu amilifu. Katika sura hii, tumeshughulikia masuala muhimu ya kifeministi yanayodhihirisha ukinzani. Kimsingi, tumechunguza mawasilisho kinzani ya masuala ya kifeministi. Vile vile, tumeeleza jinsi mivutano ya kitamaduni na mpito wa wakati husababisha kuwepo kwa ukinzani wenyewe.

## **SURA YA TATU**

### **WAHUSIKA: MISIMAMO, MAAMUZI NA MASUALA YA KIFEMINISTI YANAYOENDELEZWA KATIKA MAHUSIANO YAO**

#### **3.0 UTANGULIZI**

Wahusika ni viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na msanii ili msanii awatumie kama sauti ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira anayoilenga. Katika kazi za kihalisia wahusika huwa vielelezo wa binadamu wa ulimwengu halisi ingawa si lazima sifa zao zote zifungamane na zile za binadamu wa ulimwengu halisia. Kimsingi, wahusika huainishwa kama wakuu au wasaidizi kutegemea wadhifa wao katika kazi husika ya kifasihi na kuchunguzwa kwa kuainisha sifa zao na uhusika wao. Hata hivyo uchunguzi wa wahusika unaweza kufanywa kwa kuangazia mahusiano yao na wahusika wengine

Hata hivyo wahusika huweza kuchunguzwa kwa kuangalia mahusiano baina yao na wahusika wengine au hata kati yao. Vile vile, wahusika huweza kuchunguzwa kwa misingi ya majukumu mbalimbali wanayoyatekeleza katika jamii, nafasi zao, misimamo na maamuzi wanayofanya ambayo yanadhihirika kupitia kwa mahusiano yao. Uchunguzi wa wahusika kwa misingi hii huibua masuala ya kifeministi. Katika uchunguzi huu, kumeibuka misimamo, mielekeo na maamuzi tofauti ya wahusika na baadhi ya hayo yamedhihirisha mwelekeo wa kukinzana. Katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* mawasilisho wa mitazamo kinzani ya wahusika kuhusu masuala ya kifeministi yamedhihirika. Kimsingi, hali inayojitokeza inaweza kuelezwa kama mawasilisho ya mitazamo kinzani ya wanawake kuhusu masuala ya kifeministi.

Suala kuu hasa linaloibua mitazamo na maamuzi kinzani ni suala la mahusiano. Katika mahusiano yao, wahusika huchukua nafasi, majukumu na kufanya maamuzi tofauti kuhusiana na suala la ufeministi. Mahusiano yao huelekezwa na hadhi zao za kielimu, kikazi na kijamii na hudhirisha maamuzi tofauti tofauti kuhusu masuala ya ufeministi. Maamuzi ya wahusika kuhusu masuala ya kifeministi hutekelezwa kulinganana na hadhi zao za kielimu, kikazi na kijamii. Hii ina maana kwamba wahusika watafanya uamuzi kuhusu masuala ya kifeministi kutegemea hadhi zao za kielimu, kikazi na kijamii. Jumla ya masuala haya yanaendelezwa katika jamii yenye mivutano ya kitamaduni na ya mpito wa wakati kwa hivyo mikinzano huibuka ambapo wahusika wanachukua miegemeo inayokinzana.

Kimsingi, wahusika katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* wamegawika katika vikundi viwili kulingana na hadhi zao za kielimu, kikazi na kijamii. Hadhi hizi zinawashurutisha kutekeleza majukumu, kuchukua misimamo na kufanya uamuzi wa kuafikiana na hadhi zao. Kwa upande mmoja tunao Ramatulayi na Aisatu; wawili hawa ni huru, wamepata elimu ya kisasa, wana nguvu za kiuchumi na wamejitambua kibinafsi. Isitoshe, wamekabiliana na matatizo ya kitamaduni, kifamilia na kiuchumi yanayokaribiana kupitia kwa waume wao kuo wake wa pili na kuishia kwa kutekelezwa kwa Ramatulayi na kutalikiwa kwa Aisatu.

Wahusika wengine wanaohusiana nao ni Farmata, mwanamke jirani yake Ramatulayi ambaye ni malenga- mwimbaji na mshirikina aliyekolezwa na utamaduni. Mhusika mwingine anayeafikiana nao ni Jackline, mwanamke wa Kiivori ambaye kutokana na dhuluma za mumewe na mivutano ya kidini na kijamii anajipata katika hali ya kusongwa

kimawazo kiasi cha kumdhuru kiafya. Wa mwisho ni Daba, bintiye Ramatulayi ambaye mwanzoni anapinga uamuzi wa mamake wa kubaki katika ndoa iliyomdhalilisha hatimaye akaja kumwelewa mamake, kumuauni anapokalifika na ulezi wa wanawe na kumtia moyo. Mtazamo wake kuhusu ndoa ni wa kisasa.

Kwa upande mwingine, tunao wake wenza wao Ramatulayi na Aisatu ambao ni Binetuu na Nabu mdogo. Wanawake hawa wanadhihirisha ukale katika uamuzi wao kuhusu ndoa. Wanakuwa kama vielelezo vya wanawake wanaowakwaza wanawake wenzao. Viwango vyao vya elimu pia si vya juu kama Ramatulayi na Aisatu. Mbali na wake wenza wao Aisatu na Ramatulaye, tunao Shangazi Nabu na Bibi Mama-mkwe; Bibi Mama-mkwe ni mamake Binetu mke mwenza wa Ramatulayi na Nabu ni mama mkwe wa Aisatu. Wawili hawa wamekolezwa ukale wa kutosha na mitazamo yao kuhusu elimu, ndoa na ulezi inakinzana na ya Ramatulayi na Aisatu.

Wahusika wengine wanaohusiana nao ni Modu Falli, mumewe Ramatulayi aliyemtekeleza. Yeye ni wakili na mwanaharakati anayewakilisha wafanyikazi. Maudu Ba, mumewe Aisatu aliyemtaliki. Yeye ni daktari. Tamsir, nduguye Modu Falli aliye na bibi watatu na ambaye hawajibiki katika kukidhi mahitaji ya wake zake na wanawe bali amewatwika wake zake mzigo huo. Inadhihirika kwamba Tamsir hawezi kutosheleza mahitaji ya familia yake kwa hivyo ni jambo la kushangaza anapomtaka Ramatulayi akubali kuolewa naye. Dauda Dieng ni daktari pia ni mwanasiasa aliyemchumbia Ramatulayi kabla ya ndoa yake kwa Modu kisha akaja kumchumbia Ramatulayi tena baada ya kufiwa na mumewe. Mawifi zake Ramatulayi pia wapo katika kikundi hiki. Wa mwisho ni Imam; yeye alisimamia shughuli zote za mipango ya arusi ya Modu. Wote

hawa wanajumuika katika kikundi hiki cha pili kulingana na mitazamo yao ya kikale na viwango ambayo inakinzana na yale ya wahusika wa kikundi cha kwanza.

Mahusiano kati na miongoni mwa wahusika katika jamii yenye mivutano ya kitamaduni huibua mitazamo tofauti tofauti kuhusu masuala ya kifeministi. Kwa upande mwingine, mpito wa wakati umesababisha mitizamo na mikabala tofauti ya masuala haya. Pamoja na hayo, njia za kusuluhisha matatizo ya kijamii na kukabiliana na masuala ya kijamii zinatofautiana. Mahusiano ya wahusika huendelezwa kuafikiana na hadhi zao mbali mbali za kielimu, kikazi na kijamii. Mahusiano ya wahusika katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* yanadhihirisha uchangamano kutokana na mivutano ya kitamaduni na ya mpito wa wakati inayotanda. Hali hii inasababisha kuwepo kwa ukinzani baina ya wahusika; ambapo wanayakabili masuala ya ufeministi kwa njia zinazokinzana. Kielimu, inadhihirika kuwa kuna wahusika ambao wameelimika kwa upande mmoja na wasioelimika kwa upande mwingine. Kikazi, kuna wahusika ambao wana kazi kwa upande mmoja na wasiofanya kazi kwa upande mwingine. Kijamii, wahusika wahusiana kutegemea majukumu yao ya ndoa, malezi na unyumba. Masuala ya ufeministi yanaendelezwa kwa ukinzani kwa njia zifuatazo;

### **3.1 MAHUSIANO BAINA YA RAMATULAYI NA AISATU; USASA, UHURU, UHURU WA KIUCHUMI, UJITAMBUZI NA UWAJIBIKAJI**

Ramatulayi na Aisatu ni rafiki wa tangu utotoni, wanapitia dhuluma sawa katika jamii yenye ubabedume, wote walipata elimu ya kisasa ambayo inawapa nguvu za kiuchumi na kuwatoa kutoka ukale na kuwapa usasa; usasa wao unadhihirika kupitia malezi ya watoto wao. Ramatulayi anawapa binti zake uhuru wa kuenda sinema peke yao, kutangamana na



wavulana na kuvalia suruali. Usasa wake pia unajitokeza katika njia za kuwaadhibu wanao ambapo kinyume na kutumia vitisho au kiboko kama alivyotarajiwa, alitumia mbinu ya kisasa ya kuwasikiliza wanawe, kuwaelekeza na kuwahimiza. Usasa wake Aisatu unadhihirika kupitia anavyoamua kupanga nyumba na kuwalea wanawe wavulana peke yake na kupitia kwa ukweli kwamba anaendesha. Kutokana na hali kwamba wameelimika, wanapata uhuru wa kiuchumi na uwezo na kujitegemea. Uhuru huu wa kiuchumi unawapa uwezo wa kujipa uhuru kutokana na dhuluma za kiubabedume. Mahusiano baina yao yanadhihirisha ukomavu wa urafiki baina ya wanawake ambapo wanawake wanainuana. Ramatulayi na Aisatu ni vielelezo vya mwanamke kumwinua mwanamke mwenzake. Ramatulayi anaeleza;

Wewe, sonara, ulijinyima na ukanisaidia wakati wa dhiki. (Uk. 98)

*You, the goldsmith's daughter, gave me your help while depriving yourself. (Pg. 56)*

Kwa maoni yangu, uvaaji wa suruali ulikuwa unatisha kama mtu hukuwa na unene uliozidi kama ule wa kina mama wa kimagharibi. Suruali hufanya maungo yaliyonenepa ya mwanamke wa kiafrika yajitokeze, hasa matako yaliyoviringika kama tufe. Mimi lakini sikuvutiwa na mkumbo wa kuvaa mtindo huo uliombana mvaaji bila ya kumpa nafasi. (Uk. 137)

*I considered wearing trousers dreadful in view of our build, which is not that of slim western women. Trousers accentuate the ample figure of the black woman and further emphasize the curve of the small of the back. But I gave in to the rush towards this fashion, which constricted and hampered instead of liberating. (Pg. 81)*

Mahusiano baina yao ni njia ya kujiinua inayowasaidia wanawake kukuza ujitambuzi wao wa kibinafsi na kuwawezesha kutatua shida zao. Aisatu anapomtaliki mumewe anajizamisha katika vitabu na masomo ndiyo yalimwoko na kumpa nguvu.

Mahusiano baina ya Ramatulayi na Aisatu kwa msingi wa kikazi yanaendelezwa kwa uelewano mkubwa unaotokana na sababu kwamba wana kazi rasmi zinazowapa riziki na wanalazimika kuwajibikia majukumu nyumbani hata ingawa wana majukumu mengine ya kikazi. Ramatulayi na Aisatu wana tajriba sawa za kikazi hasa tangu walipofunza pamoja shuleni. Tajriba hizi za kikazi zinawapa uwezo wa kutangamana katika viwango sawa na kwa uelewano mkubwa.

Na ukaondoka. Ulikuwa na ujasiri wa unaoshangaza kwa kuyakabili kikamilifu yale maafa yaliyokupata. Uwezo uliomo kwenye vitabu... Yale ambayo jamii ilikunyima, vitabu vikakupa: baada ya kufaulu mitihani yako, nawe pia vitabu vikakupeleka Ufaransa. (Uk. 61)

*And you left. You had the surprising courage to take your life into your hands... The power of books... What society refused you, they granted: examinations sat and passed took you also to France. (Pg. 33)*

Wala hukuwa na wasiwasi na Maudu. Kwa hakika ulikuwa pale, maafa uliyoyapitia umeyakanyaga chini ya kisigino chako. (Uk. 64)

*You did not care about Maudu. Yes, indeed, there you were, the past crushed beneath your heel. (Pg. 35)*

Wengine wakakutishia: Wavulana hawawezi kufaulu bila baba yao.

*You were threatened through your flesh: 'Boys cannot succeed without their father.'*

Ramatulayi na Aisatu wanakumbana na matatizo sawa ya kijamii wakati Maudu Ba anapomtali Aisatu naye Modu Falli anamtelekeza Ramatulayi wanawake hawa wanabaki na majukumu ya kuwalea wanao peke yao. Hatimaye Ramatulayi anakuwa mjane. Wote wawili ni waathiriwa na ndoa za mitaara. Aisatu anaelewa uchungu wa Ramatulayi kwa sababu yeye mwenyewe alipita hali hiyo. Wanadhihirisha uasilia wa mshikamano na wanawake unaowapa nguvu na kutiana nguvu na kujipa moyo wakati wa shida.

### **3.2 MAHUSIANO BAINA YA RAMATULAYI, BINETUU NA NABU MDOGO; USASA NA UKALE WA NDOA NA USASA NA UKALE WA ELIMU**

Ramatulayi ameeelimika na ni kielelezo cha mwanamke anayejitambua. Isitoshe, elimu imempa uhuru na kiuchumi. Binetuu ni mwanamke na kisasa lakini aliyedhibitiwa na ukale. Binetuu anawacha ndoto zake za elimu na kuolewa na Modu Falli ambaye tayari alikuwa mumewe Ramatulayi kama mke wa pili. Kwa hivyo Binetuu anakuwa kama mwanamke ambaye anakwaza juhudi za mwanamke mwenzake kujiendeleza. Binetuu anatupilia mbali uhuru wake na uhuru wake wa kiuchumi na kuwa mtegemezi wa mwanaume. Hajali kuhusu mwanamke mwenzake. Hivi, Binetuu anabainika kama mwanamke wa kisasa ambaye anakumbatia ukale wa ndoa na elimu kwa kubali kuolewa kama mke wa pili na kukatiza elimu yake na kujiingiza katika ndoa kama mke wa pili. Mahusiano baina yao yanaonyesha ubinafsi wa Binetuu. Kwa sababu hii, Binetuu anadhihirika kama mwanamke anayeegemea upande wa ubabedume. Anapomwoa Binetu, Modu anamwachia Ramatulayi majukumu yote ya ulezi. Mahusiano baina yao yanatawaliwa na hila, kwa upande wa Binetuu kwani urafiki baina yake Binetuu na Daba, bintiye Ramatulayi ndio yalimfanya akamfahamu Modu na kuishia kuolewa naye. Isitoshe, anamfanya Modu Falli atelekeze majukumu yake kwa Ramatulayi huku kwa upande wake yeye na mamake wanapita pita mjini kwa magari makubwa makubwa. Katika maelezo yake Ramatulayi;

Kwa hiyo nilikueleza bila kukuficha hali hiyo ya kuhuzunisha ya maisha yetu, wakati ambapo Bibi Mama-mkwe alikuwa anazitembelea pembe zote za mji akitumia gari la Modu, na Binetuu alikuwa anatamba katika barabara zote akiendesha gari la aina ya Alfa-Romeo, mara jekundu, mara jeupe. (Uk. 56)

*I told you then, without any ulterior motive, of this painful aspect of our life, while Modou's car drove Lady Mother-in-law to the four corners of town and while Binetou streaked along the roads in an Alfa Romeo, sometimes white, sometimes red. (Pg. 97)*

Binetou alikuwa mwana kondoo aliyetolewa kama sadaka kwenye madhabahu ya mali... (Uk. 72)

*Binetou, like many others, was a lamb slaughtered on the altar of affluence... (Pg. 41)*

Binetuu, msichana aliye na umri ulio sawa na wa binti yangu Daba sasa alipandishwa hadhi kuwa mke mmwenzangu ambaye niliwajibika kuhusiana naye. (UK. 71)

*Binetou, a child the same age as my daughter Daba promoted to the rank of my co-wife, whom I must face up to. (Pg40)*

Ramatulayi kwa upande wake anachukizwa na kuwepo kwa mke mwenzake, anachukizwa na namna ambavyo mawifi zake walichukulia miaka yake thelathini ya ndoa kuwa sawa na miaka mitano ya Binetuu. Kimsingi, Ramatulayi na Binetuu wanatofautiana katika hadhi zao pia kielimu, kikazi na kijamii. Hali hii inasababisha wasiwe na itifaki njema na kuwasawiri kama wanaoelekea pande mbili tofauti. Ni katika mahusiano yao ndipo tunaona wazi tofauti za misimamo baina ya wanawake hawa wawili na kuibua kwa ukali hali ya mwanamke kumsababishia mwanamke mwenzake dhuluma.

Kwa upande wa Nabu mdogo, Ramatulayi, Aisatu na Nabu mdogo wameelimika na wote wana kazi wanazowajibikia. Mbali na kuwa na kazi hizi, wanalazimika kuwajibikia majukumu ya nyumbani wanapotoka kazini. Ukweli huu unawapa msingi wa kutangamana kwa kiwango sawa na kuwa a na hali ya mwanamke anayefanya kazi kutarajiwa na jamii kutosheleza majukumu yake yote mengine ya nyumbani.

Isitoshe, Nabu mdogo alikuwa na ujuzi wa kazi. Hakuwa na muda wa kupoteza hivi hivi. (Uk. 86)

*And then young Nabou had a profession. She had no time to worry about her 'state of mind'. (Pg. 49)*

Hakuna urafiki kati ya Ramatulayi na Aisatu na Nabu mdogo lakini mahusiano baina yao yanaendeleza kiwango fulani cha uwajibikaji na uelewano kutokana na elimu yao. Tofauti baina yao ni kwamba Nabu mdogo ameeelimika lakini hana uhuru wa kujitambua nje ya utamaduni na jamii aliolelewa humo. Anajipata katika ndoa ambapo mumewe analazimika kumwajibikia kwa kuwa hakutaka kumvunja moyo mamake. Isitoshe, ndoa baina yake na Mawdo Ba haikumsababisha Maudu kuwacha majukumu yake kwa wanawe Aisatu. Mahusiano baina yao yanatofautiana na yale ya Ramatunlaye na Binetu kwa kuwa hata ingawa Nabu mdogo anaharibu ndo baina ya Aisatu na Maudu Ba, wote watatu wana tajiriba zinazokaribiana kwa sababu ya hadhi zao za kielimu na kikazi. Hata hivyo, Binetuu na Nabu mdogo wanaishi maisha yanayodhibitiwa na utamaduni, wasiyojidhibiti kwa kubali kuzingatia ukale.

Nabu mdogo alitambua wajibu wake na alitii dhamiri yake kama wewe, na kama mimi! Kama hakuwa shoga yangu matatizo yetu mara nyingi yalifanana. (Uk. 87)

*Young Nabou, responsible and aware, like you, like me! Even though she is not my friend, we often shared the same problems. (Pg. 50)*

### **3.3 MAHUSIANO BAINA YA RAMATULAYI NA AISATU NA BIBI MAMA-MKWE PAMOJA NA SHANGAZI NABU; USASA NA UKALE WA NDOA, USASA NA UKALE WA MALEZI, MVUTANO WA VIZAZI, CHANGAMOTO ZA KUACHA UKALE NA KUKUMBATIA USASA NA USASA NA UKALE WA ELIMU**

Kimsingi, Ramatulayi na Aisatu wameelimika na wana uhuru na usasa huku Bibi Mama-mkwe na Shangazi Nabu hawajaelimika na ni vielelezo vya utamaduni na ukale. Kwa

sababu hii wao wanahusiana katika viwango vinavyotofautiana sana kielimu, kikazi na kijamii. Vikundi hivi viwili vinawakilisha vizazi viwili tofauti hivyo basi kunadhihirika mivutano baina yao.

Mahusiano baina ya wanawake katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* yanadhihirisha uadui wa wanawake na ubinafsi wa Bibi Mama-mkwe anayemsababisha binti yake kumchukua bwana wake Ramatulayi na kumwacha Ramatulayi na watoto kumi na wawili. Kwa kufanya hivi, Bibi Mama-mkwe anaegemea upande wa ubabedume unaolazimisha ndoa za mitaala kwa wanawake; mtazamo huu wa ndoa ni wa kikale. Nia yake kuu ilikuwa ya kuboresha hali na hadhi ya maisha yake. Yeye anakuwa kielelezo cha mahusiano yaliyovunjika baina ya wanawake wawili wakubwa na uharibifu na urafiki baina ya wanawake wawili wadogo. Kwa sababu ya kukosa elimu, Bibi Mama-mkwe haoni umuhimu wowote wa elimu. Msukumo wake maishani unatokana na haja ya kutosheleza mahitaji yake ya kimsingi ndiposa Modu Falli anapomtaka bintiye, anamshinikiza akubali kuolewa naye. Bibi Mama-mkwe aliona kwamba ndoa hii ingefungua njia yake ya kuboresha hadhi ya maisha yake na kupata hadhi ya juu katika jamii.

Athari kubwa ya ukale inajitokeza katika muhusiano baina ya Aisatu na Shangazi Nabu. Tangu mwanzo, Shangazi Nabu hakufurahia ndoa ya Aisatu na Mawdo Ba kwa kuwa Aisatu alitoka tabaka la chini kuliko Mawdo. Fununu zilienea mjini kuhusu ndoa hii kwamba;

‘Shule inawageuza mabinti zetu kuwa mashetani wanaowapotosha wanaume.’ (Uk. 36)

*'School turns our girls into devils who lure our men away from the right path.'* (Pg. 17)

Basi Shangazi Nabu akatafuta njia ya kulipiza kisasi. Kisasi chake alilipiza kwa kumletea Mawdo Ba mtoto wa ndugu yake Nabu mdogo amwoe kwa masingizio ya kwamba alikuwa anahitaji mtoto wa kumsaidia. Kwa hali hii, Nabu-sawa na Bibi Mama-mkwe-anaegemea upande wa ubabe dume unaompa mwanamume uwezo wa kuoa wake wengi. Nabu anakuwa kielelezo cha mwanamke anayevunja uhusiano baina ya wanandoa hasa waliooana kwa misingi ya mapenzi na viwango vyao vya elimu vinavyoafikiana. Shangazi Nabu anadhihirisha chuki kwa mwanamke kupata elimu ya viwango vya juu ndio maana alisisitiza maadili katika malezi ya Nabu mdogo. Hakika alimlea Nabu mdogo akimfunza unyenyekevu kwa mwanaume na maadili mengine ya kikale, alijikita zaidi katika kumfunza maadili kuliko elimu ya kisasa. Hii inadhihirika katika kauli hizi;

Nami najiuliza kwa jinsi mwanamke anaweza kujijengea maisha yake kwa kupiga domo tu tangu asubuhi hadi jioni. (Uk 57-58)

*In fact, I wonder how a woman can earn a living by talking from morning to night.* (Pg. 30)

Athari ya shule haikuwa kubwa kwa Nabu mdogo kwa vile Shangazi Nabu alihakikisha kwamba katika kutimiza lengo lake la kulipiza kisasi ilibidi amwandae binti huyo kwa namna ambayo ingalilingana na shabaha zake na wala hakutoa nafasi kwa athari nyingine yoyote. (Uk. 85)

*School had not left a strong mark on young Nabou preceded and dominated as it was by the strength of character of Aunty Nabou, who, in her rage for vengeance, had left nothing to chance in the education she gave her niece.* (Pg. 49)

Elimu simulizi hii, ambayo hueleweka kwa urahisi na imechangamka, ina uwezo wa kuiathiri dhamiri ya mtu mzima ambaye atahusishwa...upole, wema, utii, ujuzi wa kutenda vilimfanya Nabou mdogo awe msichana wa kupendeza. (Uk. 86)

*This kind of oral education, easily assimilated, full of charm, has the power to bring out the best in an adult mind...softness, generosity, docility and politeness. (Pg. 49)*

Dharau ya Shangazi Nabu kwa Aisatu inajitokeza, anamwona Aisatu kama aliyempotosha Maudu na anatahadhari Nabu mdogo asiathiriwe na usasa huo. Shangazi Nabu anamyima mwanamke haki ya kufikia viwango vya juu vya elimu na kazi hivyo basi kumnyima uhuru wa kiuchumi. Isitoshe, Shangazi Nabu na Bibi Mama-mkwe ni wawakilishi wa kizazi cha kwanza ambao wanashikilia ukale wa ndoa, ukale wa suala la malezi, udhibiti wa mwanamke na kupuuza umuhimu wa viwango vya juu vya elimu. Ramatulayi na Aisatu nao wanaendeleza usasa ndoa, elimu na malezi. Wakiwa wawakilishi wa kizazi cha pili na daraja ya mpito wa kutoka ukale na kuingia usasa wanadhihirisha mivutano iliyopo baina vizazi; mivutano imeshamiri baina ya kizazi chao na cha kwanza kwani ni katika kizazi chao ndiko kunajitokeza changamoto za kuacha ukale na kukumbatia usasa huku wawakilishi wa kizazi cha kwanza wameshikilia maadili ya ukale kuhusu ulezi, uhuru wa mwanamke, ndoa na elimu.

### **3.4 MAHUSIANO BAINA YA AISATU NA RAMATULAYI NA WAUME WAO; MIVUTANO YA USASA NA UKALE WA NDOA NA JUKUMU LA WANANDOA KATIKA ULEZI**

Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii* imejikita katika jamii ya Kiafrika na dini ya Kiislamu. Hali hii inawasilisha uchangamano wa mahusiano baina ya wanawake na wanaume. Sababu ya kuwepo kwa hali hii ni kuwa dini inampa mwanaume nguvu zaidi ya mwanamke. Ukweli huu unajitokeza katika hatua ya Modu kumwoa mke wa pili Binetuu na kumtekeleza Ramatulayi na Ramatulayi na Modu ni wanandoa na wanatangamana kama mume na mkewe. Hata baada ya kumtekeleza Ramatulayi kwa kutotaka kuenda nje



ya utamaduni-anaamua kubaki katika ndoa yake. Hakika, ni kwa kuwa Ramatulayi ameelimika hivyo basi kuwa na uwezo wa kiuchumi ndiko kulimwezesha kujiendeleza na kuwalea wanawe. Inashangaza kidogo kwamba Modu ambaye ameelimika pamoja na kuwa ni mwakilishi na wafanyikazi anashindwa kudhibiti uamuzi wake kiasi cha kutelekeza majukumu yake anapomwoa mke wa pili.

Mahusiano baina ya Modu na Ramatulayi yanadhihirisha mwafikiano wa viwango vyao vya elimu lakini nguvu za kidini na kitamaduni zimepewa nafasi kubwa kwa upande wa Modu. Dini na utamaduni unampa nguvu na uwezo wa kumwoa mke wa pili. Ndoa hii ya Modu na Binetuu inavunja uhusiano baina ya Modu na Ramatulayi huku ikimwacha Ramatulayi akiwaza jinsi ya kujiendeleza kama mwanamke pekee na namna ambavyo angewalea wanawe kumi na wawili. Ni katika urafiki wake na Aisatu ndiko anakopata nguvu za kuendelea. Modu anamsaliti Ramatulayi hivyo basi anadhihirisha mahusiano yenye maendeleo ya kurudi nyuma, anajaribu kuafikiana na ukale kwa wakati wa mpito kutoka ukale na kuingia kwa jamii katika usasa. Anakuwa mfano wa mwanaume anayemsababishia mwanamke dhuluma za kiubabedume. Ni kielelezo hasa cha babedume. Ramatulayi anaeleza jinsi ambavyo kama wanawake, waliacha ndoto zao za masomo na kukumbatia ndoa zao ambazo ziliishia kuvunjika. Anasema;

Baadhi ya wanaume wakatulalamikia kwamba tulikuwa hatuwajali. Wengine wakatuita mashetani wa kike. Lakini wengi wao walitaka kutuo. Ndoto ngapi zimetuhangaisha kuhusu nani wangeweza kutujengea maisha mazuri ya kudumu lakini watu hao tuliwadanganya tukawakumbatia wengine ambao walikuja tulipukia kama mapovu ya sabuni na kutuacha povu tupu? (Uk. 32)

*Men would call us scatterbrains. Others labelled us devils. But many wanted to possess us. How many dreams did we nourish hopelessly that*

*could have been fulfilled as lasting happiness and that we abandoned to embrace others, those that have burst miserably like soap bubbles, leaving us empty handed? (Pg. 15)*

Hata kule kuniletea mke mwenza katika maisha yangu hakukumridhisha. Kwa kumpenda mwanamke mwingine akawa ameunguza historia yake mwenyewe kimali na kimaadili. Akathubutu kunikana... kumbe. (Uk. 28)

*This addition of a rival into my life was not enough for him. In loving someone else, he burned his past, both morally and materially. He dared to commit such an act of disavowal. (Pg. 13)*

Anajikufuru kutosheleza mahitaji yote ya Binetuu ambaye anapandisha matakwa yake kila uchao ili iwe kama fidia ya uhuru wake aliotoa kafara kwa matamanio ya mamake katika ndoa asiyoipenda. Anamtelekeza mke wake wa kwanza na kumtwika majukumu yote huku anajijasirisha kukidhi mahitaji ya mama-mkwe na mkewe na pili. Mahusiano haya yanaonyesha dhuluma kwa mwanamke ambazo zina kiini chake katika utamaduni, na hasa mwanaume asiyetaka kuwajibika. Haya yote yanasababaisha kutatizika kwa mahusiano baina yao.

Kwa upande wake Aisatu na mumewe Mawdo wameelimika na Aisatu ana kazi na Mawdo ana kazi ya udaktari. Mawdo anapomwoa mke wa pili, anaendelea kutekeleza majukumu yake kwa Aisatu lakini Aisatu hakutaka kubaki katika ndoa ile. Mawdo anapokabiliana na pendekezo la mamake, anadhihirika kuwa asiye na uwezo wa kufanya uamuzi wa kukataa kumwoa Nabu mdogo. Aisatu anaondoka baada ya kumtaliki Mawdo na kujiingiza katika masomo. Hakika, chanzo cha dhuluma za kijamii alizopata Aisatu si Mawdo bali ni Shangazi Nabu. Mahusiano ya Mawdo na Modu yanadhihirika kama yaliyosababisha kuvunjika na mama-mkwe ambaye kwa sababu za ukale ana kisasi na mkaza-mwana wake. Mawdo anahusika katika kuvunjika kwa uhusiano wake na Aisatu hadi tu pale pa kumruhusu mamake kumshinikiza amwoe Nabu mdogo akisingizia

kwamba ni kwa sababu ya kumjali mamake ndipo anakubali kumwoa Nabu kwani hakumpenda. Tazama kauli hii;

Ni kwa ajili ya 'kutomwona mamake anakufa kwa aibu na hasira' ndipo Mawdo alipokubali kuenda kukutana naye kimwili usiku wa arusi. (Uk. 58)

*It was 'so as not to see his mother die of shame and chagrin' that Mawdo agreed to go to the rendezvous of the wedding night. (Pg. 31)*

Hivyo basi, Mawdo anaharibu uhusiano wake na Aisatu katika ndoa iliyokuwa na msingi wake kwenye mapenzi na maafikiano ya kielimu na kujiingiza katika uhusiano wa ndoa na Nabu mdogo ambaye amelelewa kwa nia ya kumtosheleza Mawdo kama mke aliyeelimika lakini aliye na ukale wa kutosha.

### **3.5 MAHUSIANO BAINA YA RAMATULAYI NA FARMATA; UKALE WA NDOA, NDOA YA MITAALA NA ULEZI**

Farmata ni mwanamke wa tabaka la chini asiyeelimika na aliye na ukale. Farmata anaona kwamba ana mchango katika uamuzi wa Ramatunlaye kuhusu ndoa na katika ulezi wa wanawe Ramatulayi. Hata hivyo, Ramatulayi ana mkabala tofauti naye kuhusu baadhi ya mambo kama vile ndoa; anakataa kuolewa na Dauda huku Farmata anamshinikiza akubali. Wanatofautiana kuhusu ulezi na njia za kuwaadhibu watoto wanapokosea; baada ya kugundua kuwa bintiye alikuwa mja mzito Ramatulayi anamwelewa bintiye, anamkinga na kumtia moyo huku Farmata akitarajia kwamba angemzomea na kumsuta au hata amwadhibu kuhusu Ibrahima Salli aliyemtunga mimba Aisatu. Farmata alitaka Ibrahima atambue kosa lake na anamsuta na kumwambia awaeleze wazazi wake kwamba walifaa kumfidia Aisatu. Hata hivyo, Ramatulayi hakujishughulisha sana na hayo bali alilipa uzito wazo la elimu kwa bintiye aliwaza ikiwa bintiye angefukuzwa shuleni.

Inabainika kwamba muhusiano yao yanasababisha njia zao za kusuluhisha mambo na maamuzi yao kutofautiana kwa sababau ya ukale na kutoelimika kwa Farmata na usasa na elimu ya Ramatulayi. Ramatulayi anaamua kutoolewa tena na kuchagua uhuru pale ambapo Farmata anamkumbusha kwamba anahitaji mwanaume. Farmata amejikita katika utamaduni na ndio unamfanya aamini kwamba ana mchango mkuu katika maamuzi ya Ramatulaye kwa kuwa ndiye mmoja wa wanawake wakubwa wa tabaka hilo. Kimsingi tofauti za usasa na ukale zinajidhihirisha katika mahusiano yao. Farmata anatumia ushirikina kupiga ramli na kumfahamisha Ramatulayi kuhusu mwanaume tajiri ambaye anamtaka Ramatulayi amkubali. Ramatulaye anaeleza alivyoambiwa na Farmata;

... ananijia ‘mwanaume aliyevaa suruali mbili, ahadi ya utajiri’ (Uk. 74)

... *‘the man in the double trousers is coming towards me, the promise of wealth.’ (Pg. 42)*

Bahati yako unaitupa nje. Dauda Diengi ni tajiri, mbunge, daktari, mtu wa rika lako, tena ana mke mmoja tu. Anakupatia usalama wa mapenzi nawe unakataa! (Uk. 124)

*You trample upon your lack: Daouda Dieng, a rich man, a deputy, a doctor, of your own age group, with just one wife. He offers you security, love, and you refuse! (Pg. 73)*

### **3.6 MAHUSIANO BAINA YA RAMATULAYI NA DABA; USASA WA NDOA, UJITAMBUZI WA MWANAMKE, KUSHIRIKI KWA MWANAMKE KATIKA SIASA NA UONGOZI, MAJUKUMU YA UNYUMBA NA UHURU WA MWANAMKE**

Daba, bintiye Ramatulayi mwanzoni alipinga uamuzi na mamake, kwa kubaki katika ndoa yake lakini mwishowe akawa ndiye anamtia moyo mamake na kumwauni wakati wa kugawa mali ya Modu. Watoto wake Ramatulayi walikuwa kama kizingiti kwake; walimpa sababu ya kuishi. Daba alitokea kuwa kielelezo cha mahusiano makomavu baina

ya mwanamke na mwanamke mwenzake ambapo mwanamke anamsaidia mwanamke kujiendeleza. Ana uelewa kuhusu nafasi anayopewa mwanamke katika jamii na ile ambayo mwanaume amepewa kijamii.

Na huku wanangu wote kwa pamoja wakiwa wamekataa kutokana na jinsi walivyoshawishiwa na Daba. (Uk. 83)

*And to my family's great surprise, unanimously disapproved of by my children who were under Daba's influence. (Pg. 47)*

Walishaendesha majadiliano kadhaa kwa ajili ya ugawanaji wa mali za Modu. Mkwe wangu aliweka mezani malipo ya mwanzo kwa ajili ya nyumba ya SICAP na jumla yote ya miaka mitano ya kodi ya nyumba. (Uk.126)

*They had led the fight for the distribution of Modou's estate. My son-in-law laid down on the table the advance for the SICAP villa and five year's rent. (Pg. 74)*

Ebu kumbuka mimi nilikuwa shoga mpenzi wa binti yako. Wewe ukamfanya awe mshindani wa mama yangu. Kumbuka. Kwa muda wa miaka mitano umewanyang'anya mam na wanawe kumi na wawili msaada waliokuwa wanauhitaji sana. Kumbuka. Mama ameteseka kweli kweli. Inawezekanaje mwanamke amharibie mwanamke mwenzake bahati yake? (Uk. 127)

*Remember I was your daughter's best friend. You made her my mother's rival. Remember. For five years you deprived my mother and her twelve children of their breadwinner. Remember. My mother has suffered a great deal. How can a woman sap the happiness of another? You deserve no pity. Pack up. (Pg. 74)*

Ramatulayi anaonea fahari uhusiano wa bintiye Daba na mumewe Abdu ambao kwa kila hali wanaendeleza usasa wa ndoa na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya unyumba. Tofauti na mtazamo wa kikale, wa kiubabedume, abdu anaona suala la upishi ni jukumu la wote na kwamba anastahili kumsaidia mkewe. Kuhusu suala la ndoa, Daba anadhihirisha usasa na uhuru wa mwanamke kujiondoa katika ndoa endapo itamchusha. Huu ni usasa wa kiwango cha juu kuhusu ndoa. Daba ana mawazo yake kuhusu siasa,

kwamba si lazima mwanamke ajiunge na siasa hasa kwa kuwa siasa imetawaliwa na mapendeleo ya wanaume na tamaa ya uongozi ya wanaume. Anapendekeza uongozi wa zamu, usiokuwa na mizozano ya kuwania nafasi za uongozi na ambapo kila mmoja ana haki ya kuwasilisha mawazo yake. Ni kielelezo cha mwanamke anyejitambua, ambaye yu huru na anayeendeleza usasa.

Daba hazidiwi na kazi za nyumbani. Mumewe anajua kupika wali kama yeye mwenyewe. Ninapomwambia kwamba anamharibu mkewe, yeye husema: “Daba ni mke wangu si mtumwa wangu wala mjakazi wangu.”

*Daba does not find household work a burden. Her husband cooks rice as well as she does; her husband who claims, when I tell him he ‘spoils’ his wife. ‘Daba is my wife. She is not my slave nor my servant. (Pg. 77)*

... Kila mara ananiambia: “Sitaki kujiingiza katika siasa, siyo kwa kuwa tua majaliwa ya nchi yangu hasa ile ya kina mama hainihusu, la! Nikiangalia migongano isiyo na faida miongoni mwa wanachama wa chama kile kile, na nikiangalia tama ya madaraka ijibainishayo kati ya wanaume, naona bora niisuse... “Hasha, siogopi mapambano katika usawa wa itikadi; lakini katika chama cha siasa, si rahisi kwa mwanamke kujipenyeza kwa urahisi. (Uk. 132)

Napendelea chama changu ambamo hakuna mashindano, matengano, kashifa na masukumano... Uongozi unabadilika kila mwaka. Kila mmoja wetu hupewa nafasi sawa ya kuleta mawazo yake ili yathaminiwe. (Uk. 132)

*... She often tells me: I don’t want to go into politics; its not that I am not interested in the fate of my country, and most especially that of woman. But when I see the fruitless wrangling even within the ranks of some party, when I see men’s greed for power, I prefer not to participate... No, I am not afraid of ideological struggle, but in apolitical party it is rare for a woman to make a break-through. (Pg. 78)*

*No: I prefer my own association, where there is neither rivalry or schism, neither malice nor jostling for position... The headship changes every year . Each of us has equal opportunity to advance her ideas. (Pg. 78)*

### **3.7 MAHUSIANO BAINA YA RAMATULAYI TAMSIR NA IMAMU; NDOA ZA MITAALA, UBABEDUME KUTOWAJIBIKA KWA WANAUME KATIKA ULEZI**

Tamsir–ndugu yake Modu na Imamu ndio walienda kumpasha Ramatulayi habari kuhusu kifo cha mumewe. Wawili hawa kwa kila hali ni wanaume ambao wana viwango vya chini kielimu. Ni mababadume wanaowakilisha na kuendeleza na dini na utamaduni. Imamu anamwambia Ramatulayi kwamba kwa mwanamume kuoja mke wa pili ni majaliwa ya mola na kudai kwamba hakuna cha kufanya mola anapowaweka watu wawili pamoja. Hii inadhihirisha jinsi kwa msingi wa dini mwanamke hana nguvu au uwezo anapokabiliwa na dini. Tamsir kwa upande wake anampendekeza Ramatulayi wazo la kumwoa atakapotoka katika utawa wake. Anapopendekeza hili Ramatulayi anafahamu kwamba ana wake watatu na watoto wengi. Anawaachia wake zake jukumu la kuwalea na kuwakidhi wanawe. Tamsir anawasilisha ujumbe wa Modu;

Modu anakushukuru. Anasema kwamba tu majaliwa huamua kwa ajili ya watu na vitu: Mola amemjalilia mke wa pili na hawezi kukataa. (Uk. 68)

*‘Modou sends his thanks. He says it is fate that decides men and things: God intended him to have a second wife, there’s nothing he can do about it’. (Pg. 38)*

Imamu anaonyesha kwamba anakubaliana na mawazo ya Modu. Anasema hivi;

“Mungu anapowaweka viumbe wawili mmoja karibu na mwingine hakuna mtu atakayefanya jambo lolote.”

*There’s nothing one can do when Allah the almighty puts two people side by side. (Pg. 37)*

Mahusiano baina ya watatu hawa yanadhibitiwa na dini na ukale wa Imamu na Tamsir; wanatarajia kwamba Ramatulayi atakubali mapendekezo yao bila kupinga kwa sababu ni mwanamke. Kwa upande wake Ramatulayi anachukua pendekezo hili kama kichocheo, anawasilisha mawazo yake, akamwambia msimamo wake, kuwasuta na kuwakumbusha kwamba yeye si chombo cha kurithishwa. Mahusiano yao yanakuwa mwanzo wa sauti yake kama mwanamke aliyenyamazishwa na utamaduni kwa muda mrefu na kudhalilishwa. Hakika, yanadhihirisha makabiliano baina ya mababedume kwa upande mmoja na mwanamke amabaye amejitambua na kupata uhuru wake kwa upande mwingine.

### **3.8 MAHUSIANO BAINA YA RAMATULAYI NA DAUDA DIENGI; USHIRIKISHWAJI WA WANAWAKE KATIKA SIASA**

Dauda Diengi alikuwa mchumba wake Ramatulayi kabla hajaolewa na Modu. Ameelimika, ni daktari na ni mwanasiasa. Mahusiano baina ya Ramatulayi na Dauda yanadhihirisha maafanikiano katika viwango vyao vya elimu. Mazungumzo yao yanadhihirisha uelewano na upevu wao kuhusu masuala ya kijamii na ya kikazi. Dauda ni kielelezo cha mwanaume ambaye anawajibikia majukumu yake ya kijamii ipasavyo pamoja na kuwa ni kiongozi anayewajibika. Isitoshe anadhihirisiha msimamo thabiti na maamuzi yake yanafanywa na busara. Anatambua mchango wa wanawake katika jamii na kupendekeza kwamba wanawake wanapaswa kuhimizwa kujishughulisha na maendeleo ya nchi.

Dauda kielelezo cha mwanaume ambaye anaelewa kwamba mwanamke anapaswa kujitambua. Hii inadhihirika katika hotuba zake katika bunge ambapo amepewa jina



“mfeministi” kwa sababu ya kutambua nafasi za wanawake. Kwa kunuia kupata suluhisho la dhuluma za kijamii na hata kuelewa hali halisi ya mivutano iliyomkumba Ramatulayi anatokea kuwa kielelezo cha mwanaume wa kisasa anayetambua nafasi ya mwanamke, mchango wake kisiasa, haja ya kuwahusisha wanawake katika siasa na juhudi za kujikomboa kwake. Mahusiano yao yanawasilisha mtazamo wa mwanaume kuwa sawa na wa mwanamke na kumsawiri mwanamke kama aliye na nafasi sawa na mwanaume kisiasa Kauli hizi zinathibitisha haya;

Ni mume mwema? Ndiyo. Maneno ya mitaani yenye lengo la kukashifu mtu yanayoenezwa na wanawake wambeya dhidi ya watu wakubwa, bado hayajamtoa kasoro yoyote ile. (Uk. 120)

*A good husband? Yes. Public rumour so wicked and thirsty for gossip where personalities are concerned, has never mentioned any goings-on of his. (Pg. 70)*

Alikuwa mwaminifu na kila ilipobidi alipigania haki iwepo zaidi katika jamii.(UK. 110)

*He was an upright man, and each time the situation demanded, he would fight for social justice. (Pg. 64)*

Hoja zangu ninazorudia kila mara huko Bungeni, wanakoniita “mtetea kina mama” unazijua fika. (Uk. 110)

*You are echoing my speeches at the national assembly where I have been called a “feminist”... Women should no longer be decorative accessories, objects to be moved about, companions to be flattered or calmed with promises. (Pg. 64)*

### **3.9 HITIMISHO**

Katika sura hii tumeshughulikia mawasilisho ya mitazamo kinzani ya wanawake kuhusu masuala ya kifeministi. Tumechunguza jinsi mitazamo kinzani ya wanawake na wahusika wanaume inadhihirisha ukinzani tunapochunguza mahusiano yao. Kwamba, katika mahusiano yao, wanawake na wanaume huchukua majukumu tofauti tofauti hivyo basi kufanya maamuzi tofauti kuhusu masuala ya kifeministi. Isitoshe, tumechunguza mawasilisho haya kwa kuchanganua mahusiano baina ya wahusika mbali mbali katika riwaya ya Barua Ndefu Kama Hii tukionyesha jinsi mahusiano hayo yanadhibitiwa na kuendelezwa na hadhi za kielimu, kikazi na kijamii za wahusika.

## **SURA YA NNE**

### **HITIMISHO**

#### **4.0 UTANGULIZI**

Sura hii inalenga kuangazia muhtasari wa matokeo yetu ya utafiti. Katika utafiti wetu, tumeweza kujadili masuala ya kifeministi tukiongozwa na nadharia tulizoteua kuegemea pamoja na malengo ya utafiti wetu na nadharia tete. Vile vile, tumeangazia changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti wetu pamoja na mapendekezo.

#### **4.1 KUHUSU MADHUMUNI YA UTAFITI**

Utafiti ambao tumefanya ulinuia kuchunguza uwasilishaji wa ufeministi kinzani katika Kiswahili kupitia tafsiri kwa kutathmini riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Katika utafiti wetu tuliongozwa na malengo yafuatayo ya utafiti;

Kwanza, tulinuia kuchunguza uelewa unaoibuliwa na masuala ya ufeministi katika fasihi ya Kiswahili. Tumetimiza lengo hili katika sura ya pili ambapo tumewasilisha uelewa kinzani wa ufeministi kwa kuchanganua masuala kinzani ya ufeministi katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Kwa kufanya hivyo, tumebaini kwamba uelewa kinzani wa ufeministi upo katika fasihi ya Kiswahili.

Pia, tulinuia kuchunguza namna ufeministi kinzani unavyojibainisha katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Lengo hili tumelitimiza kwa kuchunguza mahusiano baina na miongoni mwa wahusika wa riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Katika kuchunguza mahusiano haya tumebaini kwamba ufeministi kinzani hujitokeza katika mahusiano baina na miongoni mwa wahusika ambapo wahusika huchukua misimamo kinzani na kufanya

maamuzi inayokinzana kuhusu masuala ya ufeministi. Isitoshe, wahusika hutekeleza majukumu yanayotofautiana na kuyatekeleza kwa njia zinazokinzana. Ni katika sura ya tatu ndiko lengo hili limetimia.

Hatimaye tulinuia kuthibitisha kwamba ufeministi kinzani unafikishwa katika fasihi ya Kiswahili kupitia tafsiri. Uchanganuzi wa ufeministi kinzani katika riwaya tuliyoiteua umebainisha kwamba tafsiri ndiyo imewezesha ufeministi kinzani kuwepo katika fasihi ya Kiswahili. Madhumuni haya yametekelezwa katika sura ya pili na ya tatu kwa pamoja.

#### **4.2 UPIMAJI WA NADHARIA TETE**

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia tete tatu kuu:

Kwanza, masuala ya ufeministi yanaibua uelewa kinzani katika fasihi ya Kiswahili. Uchunguzi wetu umethibitisha ukweli wa nadharia tete hii. Mbali na ufeministi, kuna uelewa wa ufeministi ulio kinzani katika fasihi. Uelewa huu umeweza kufikishwa katika fasihi ya Kiswahili kupitia tafsiri. Utafiti wetu umethibitisha kwamba masuala ya utamaduni na usasa wa elimu, unyumba, usasa na ukale wa ndoa, mpito na mvutano wa vizazi, wajibu wa wanandoa katika ulezi, uhuru wa kiuchumi na utegemezi wa kiuchumi na suala la uhuru ni baadhi ya masuala ya kifeministi yanayodhihirisha ukinzani katika fasihi ya Kiswahili.

Ufeministi kinzani unajibainisha kupitia nafasi, majukumu na misimamo ya wahusika wa riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Nadharia tete hii ni kweli kwa kuwa utafiti huu ulibainisha kuwa ufeministi kinzani hujitokeza kupitia kwa mahusiano ya wahusika. Isitoshe, imebainika kwamba katika mahusiano ya wahusika, wahusika huchukua

misimamo inayokinzana, huwajibikia majukumu yao kwa njia zinazokinzana na kufanya maamuzi kinzani kuhusu suala lile lile. Utafiti wetu umebainisha kwamba mahusiano ya wahusika katika riwaya yanaibua ukinzani. Mahusiano haya yanaendelezwa na hadhi za kielimu, kikazi na kijamii. Mahusiano yanayodhihirisha ukinzani ni pamoja na;

- i. Mahusiano kati ya Ramatulayi na Aisatu
- ii. Mahusiano baina ya Ramatulayi na Binetuu na Nabu mdogo
- iii. Mahusiano baina ya Ramatulayi na Aisatu na Bibi Mama-mkwe pamoja na mama mkwe zao.
- iv. Mahusiano baina ya Aisatu na Ramatulaye na Waume wao.
- v. Mahusiano baina ya Ramatulayi na Farmata na Daba
- vi. Muhusiano baina ya Ramatanlaye Tamsir na Imamu

Utafiti wetu umebainisha kwamba wahusika wamegawika kwa vikundi viwili; Wale walioelimika, wana kazi na wana usasa na ni huru kwa upande mmoja na wasioelimika wasio na kazi au walio na ukale na wasio huru kwa upande mwingine. Katika kikundi cha kwanza kuna Ramatulayi, Aisatu, Dauda Dieng Ibrahima Sall na Daba. Kwa upande mwingine kuna Binetuu, Shangazi Nabu, Nabu mdogo, Modu, Maudo na Farmata. Modu na Maudo wamewekwa katika upande huu japo wameelimika kwa sababu ya mitizamo yao inayokinzana na Ramatulaye na Aisatu. Wao wamedhihirishwa kuwa mababedume, walioelimika, lakini wamekumbatia ukale, utamaduni na dini.

Nadharia tete ya tatu ya utafiti hii ulikuwa ukinzani wa ufeministi unafikishwa katika fasihi ya Kiswahili kupitia tafsiri. Ukweli wake umejitokeza kupitia uchanganuzi wa masuala haya kinzani ya kifeministi na uchanganuzi wa mahusiano ya wahusika

yanayoibua ukinzani wa masuala ya ufeministi. Imedhihirika kuwa tafsiri ndiyo imewezesha ufeministi kinzani kufikia fasihi ya Kiswahili.

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya ufeministi wa Kiafrika na ulinganifu amilifu. Nadharia ya ufeministi imetusaidia kueleza masuala ya kifeministi yanavyojitokeza katika muktadha wa Kiafrika. Imetupa uwezo wa kufafanua muktadha wa kiafrika pamoja na utamaduni wake unaodhibiti na kuelekeza masuala ya kifeministi katika muktadha wa Kiafrika. Kwa kugemea nadharia yenyewe tumeweza kufikia hitimisho kuhusu masuala ya ufeministi na yanavyojitokeza katika riwaya. Nadharia ya ulinganifu amilifu imetuwezesha kuchanganua ulinganifu wa kisemantiki, kimtindo na kitamaduni katika riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Imekuwa kama kielelezo cha kupimia ulinganifu wa yaliyomo.

Tumewasilisha utafiti wetu kwa njia ya maelezo yaliyoandikwa. Kazi hii imewasilishwa kwa sura tatu. Sura ya kwanza imejumuisha vipengele muhimu iliyotuongoza katika utafiti wetu. Vipengele hivyo ni; usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na msingi wa nadharia ambazo ni mbili; nadharia ya ufeministi wa Kiafrika na nadharia ya ulinganifu amilifu na mwishowe tukabainisha mbinu tutakazozitumia katika utafiti wetu. Katika sura ya pili tuliangazia mawasilisho kinzani ya masuala yanayowahusu wanawake.

Masuala haya ni pamoja na; utamaduni na usasa wa elimu, unyumba, usasa na ukale wa ndoa, mpito na mvutano wa vizazi, wajibu wa wanandoa katika ulezi, uhuru wa kiuchumi na utegemezi wa kiuchumi na suala la uhuru. Vile vile, tumeonyesha baadhi ya mivutano

iliyomo katika jamii na ambayo inaathiri uwasilishaji wa masuala haya ya kifeministi. Mivutano hiyo ni pamoja na; mivutano ya usasa na ukale, mivutano ya kitamaduni, kijamii na ya mpito wa wakati. Ni mivutano hii ndiyo inadhibiti mahusiano, maamuzi na majukumu ya wahusika na kuchochea kuwepo kwa mitizamo kinzani. Tulichunguza masuala haya kwa kuegemea nadharia ya ulinganifu amilifu na ya ufeministi wa Kiafrika ili kueleza masuala yenyewe katika muktadha wa Kiafrika na kuthibitisha kwamba yaliyomo yanahawilishwa hadi fasihi ya Kiswahili kwa ulinganifu.

Katika sura ya tatu, tumeshughulikia uchunguzi wa njia ambayo ufeministi kinzani hujibainisha kupitia kwayo ambayo ni mahusiano ya wahusika. Isitoshe, tumeeleza jinsi katika mahusiano yao wahusika huchukua misimamo tofauti tofauti na kufanya uamuzi tofauti kuhusu masuala wanayokumbana nayo. Vivyo hivyo, tumeeleza kwamba wahusika huchukua majukumu tofauti tofauti katika jamii kwa hivyo misimamo yao na maamuzi yao hutofautiana. Tumeongozwa na nadharia mbili; nadharia ya ufeministi wa Kiafrika katika kuchunguza masuala ya kifeministi na ulinganifu amilifu kuchanganua suala la ulinganifu wa yaliyomo yanapohawilishwa hadi Kiswahili.

#### **4.3 CHANGAMOTO ZA UTAFITI**

Hatukukumbana na matatizo mengi katika utafiti wetu ila tu tatizo tulilokumbana nalo katika utafiti wetu ni muda mfupi wa kusanya data tukizingatia upana wa eneo la ufeministi. Hata hivyo tuliweza kufanya utafiti wetu na kusanya data zilizotufaa katika utafiti wetu.

#### **4.4 MAPENDEKEZO**

Matumaini yetu ni kwamba utafiti wetu utakuwa msingi bora wa uchanganuzi wa ufeministi kinzani katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu ulishughulikia masuala ya ufeministi kinzani na uhawilishaji wake hadi fasihi ya Kiswahili. Tunapendekeza utafiti zaidi wa Kiswahili ufanywe kwa kujikita katika maudhui mengine ya riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*.



## MAREJELEO

- Ahikire, J. (2014) 'African Feminism in the 21<sup>st</sup> Century' in Mama, A. and Abbas, H. (eds.), *Feminist Africa: Pan Africanism and Feminism*. No. 19.
- Aiello, F. T. (2013) *Translating Culture: Literary Translations into Swahili by East African Translators*. Swahili Forum.
- Ba, M. (1994) *Barua Ndefu Kama Hii*. (Maganga, C. - Mtafsiri) Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.
- \_\_\_\_\_ (1979) *So Long a Letter*. (Modupe Bode- Thomas- Trans) London: Heinemann
- Bassnet, S. & Lefevere, A. (2001) *Constructing cultures: Essays on Literary Translation*. Shanghai: Shanghai Foreign Language Education Press.
- Bressler, C. E. (2003) *Literary Criticism. An Introduction to Theory and Practice*. Prentice Hall. New Jersey.
- Christian, B. (1985) *Black Feminist Criticism: Perspectives on Black Women Writers*. Harper and Row Publishers. London.
- Collins, P., H. (2000) *Black Feminist Thought: Knowledge, Consciousness and the Politics of Empowerment*. Routledge. Print.
- Davies, C., B. and Graves A., A., (1987). *Ngambika: Studies of Women in African Literature*. The International Journal of African Historical Studies. Vol, 20. No.1
- De Beauvoir (1957) *The Second Sex*. London: Jonathan Cape.
- Gyasi K., A. (2006) *The Francophone African Text: Translation and the Postcolonial Experience*. P. Lang. University of Michigan.
- Hermans T. (1985) (ed.) *The Manipulation of Literature: Studies in Literary Translation*. Routledge print.

- Jones, D., E. et. al. (eds.) (1985) *Women in African Literature Today*. Heinemann. London. Ibadan. Nairobi.
- Leslie, O., M. (1984). "Recreating Ourselves: African Women and Critical Transformations." Trenton. African World Press. Inc.
- Mansfield, H., C. (2014). *The Contradiction That Rules Feminism*. HOOVER INSTITUTION. Thur. Dec. 18 2014.
- Millet, K. (1970). *Sexual Politics*. Virago. London.
- Maduka C., T. (2005) *Africa and Comparative Literature in the Era of Globalization* in Chidi T. and Denis E. EDS. *Compass: Essays in Honour of Wilfred F. Feuser*. Port Harcourt.
- Masibo, B. (2009) *Gendered Perspectives in Novels of Ngugi wa Thiong'o and Alice Walker*. (Phd Thesis, University of Nairobi. Unpublished).
- Mutua, J., M. (2007) *Mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za kiswahili*. (Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).
- Mutwiri, E., M. (2013) *Literary and Untranslational Complications in the Translation of The Government Inspector from English to Kiswahili*. (PhD Thesis, University of Nairobi).
- Nnaemeka, O. (2005) *Bringing African Women into Classroom: Rethinking Pedagogy and Epistemology in African Gender Studies*. <http://mojubaolu.blogspot.com>
- Nida, E. (1964) *Towards a Science of Translating*. Leiden: E. J. Brill.
- Nida, E., A. and Taber (1969) *The theory and practice of translation*. Leiden. E J. Brill.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

- Sayed, S. (2014) "The Struggle of African Women in Selected Works by Ngugi Wa Thiong'o" *European Scientific Journal*. Vol.10. No. 5.
- Showalter, E. C. (1977) *A Literature of Their Own*. Newyork: Routledge.
- Steady, F. (1981) *The Black Woman Cross-Culturally*. Schennman. Cambridge.
- Stegeman, B. (1974) 'The Divorce Dilemma: The New Woman in Contemporary African Novels; in critique: Studies in Modern Fiction.
- Swaleh, A. (2011) *A Criteria of Mapping and Construction of Gender Identity and Authority in Selected Kiswahili Novels*. University of Nairobi. (Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi).
- The Guardian (2014) 'Sexuality in Africa' in Mama, A. and Abbas, H. (ed.), *Feminist Africa: Pan - Africanism and Feminism*.
- Toury, G. (1995) *Descriptive Translation Studies and Beyond*. John Benjamins.
- Venuti, L. (1995) *The translators invisibility: A History of Translation*. New York: Routledge.
- Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Msingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Zaja, O. (1986) *Fasihi Tafisiri Katika Ukuzaji Wa Fasihi ya Kiswahili: Matatizo na Athari zake*. (Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).
- \_\_\_\_\_ (2006) *Siting Text, Culture, Context and Pedagogy in Literary Translation*. (Phd Thesis, Kenyatta University).
- Zhang, L., Y. (2015) *Feasibility of Applying Functional Equivalence Theory to Chinese Translation of English Songs*. Vol. 10 <http://www.cscanada.net/index-php/sii/article/view/6245>